# Nipashe

Ijumaa Juni 12, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580256

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710





Mboga bila vyama vya siasa inawezekana! - 2

BUFE

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Mradi gesi kinyesi unavyohamisha wananchi kutoka umaskini wa kuni

MTAZAMO WA DUNIA

Uchumi baada corona, dira kuzalisha zaidi, mahitaji...


## Magari matatu yagongana, yaua watu wanane Mwanza

UKURASA 19

UKURASA 11

# Kicheko, kilio Bajeti 2020/21

UKURASA 2,3,4, 19




## BAA LA CORONA



Sera ya mfanyakazi kurudi kazini baada ya kuambukizwa virusi vya corona na kupona, lazima itumike sehemu za kazi. Shirika la Afya Duniani (WHO), linashauri mgonjwa aliyethibitika kupona anaweza kurudi kazini baada ya siku 14 za kujitenga na kutokuwa na dalili zozote za ugonjwa huo.

- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## IMF YAIFUTIA TANZANIA DENI BIL. 33/-

UKURASA 8



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




## Magufuli amsamehe Andengenye

UKURASA 8


MICHEZO TARIMBA AFUNGUKA KERO ZA MABADILIKO UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Kicheko, kilio bajeti 2020/21

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MAKADIRIO ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha yaliwasilishwa bungeni jijini Dodoma jana, yakiwa na mapendekezo yanayofurahisha na mengine machache kuonekana mwiba kwa baadhi ya walengwa.

Bajeti hiyo ya Sh. trilioni 34.88, ni ya mwisho kwa awamu ya kwanza ya serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli, ikiongezeka kutoka Sh. trilioni 33.1 zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha (2019/20), sababu kuu ikitajwa kuwa gharama za uchaguzi mkuu na mahitaji halisi ya ugharamiaji miradi mikubwa ya kimkakati, ulipaji mishahara, deni la serikali na vipaumbele vingine vya taifa.

Katika uwasilishaji wake, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alidokeza kodi na tozo ambazo anapendekeza zirekebishwe katika bidhaa na huduma mbalimbali zinazozalishwa ndani na nje ya nchi kama ilivyokuwa katika bajeti zilizopita.

Bidhaa zilizoguswa ni pamoja na juisi, bia pamoja na kodi kwenye sekta ya viwanda, kilimo, mifugo, madini na huduma muhimu za kijamii.

Kama ilivyoahidiwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, serikali imependekeza kuwa na punguzo la tozo, ada, kodi na ushuru kwenye sekta anazozisimamia (mifugo na uvuvi).

Serikali pia imependekeza kuondoa migongano ya sheria, kanuni na taratibu zinazotumiwa na mamlaka mbalimbali katika utozaji kodi na gharama kubwa za kuanzisha na kuendesha biashara kutokana na wingi wa kodi, ada na tozo zinazoambatana na taratibu zenye urasimu.

Miongoni mwa mapendekezo ya serikali katika bajeti hiyo ni kufuta tozo ya mafunzo ya elimu kwa umma iliyokuwa inatozwa kiasi cha Sh. 250,000 kwa kila mshiriki kwa kuwa hilo ni jukumu la msingi la OSHA kuelimisha umma.

"Napendekeza kupunguza ada ya uchunguzi wa ajali iliyokuwa ikitozwa kiasi cha Sh. 500,000 kwa kila mtaalamu anayefanya uchunguzi hadi Sh. 120,000 kwa kila mtaalamu, lakini si zaidi ya Sh. milioni moja," alisema waziri huyo.

Dk. Mpango pia alisema anapendekeza kuongeza ada ya kutunza mbuzi au kondoo kwenye vituo vya karantini, kupumzishia mifugo na ukaguzi kwa kila mmoja kutoka Sh. 200 hadi Sh. 500.

Pia, kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Mtaji (Capital Gains)kwenye mapato yatokanayo na ubadilishaji wa leseni (concessionalright) katika ardhi iliyohodhiwa na kupangishwa kwa mwekezaji mwingine.

Waziri huyo pia alisema serikali inapendekeza kufanya marekebisho kwenye makato ya mishahara ya waajiriwa, mabadiliko yakionekana kuwanufanisha wenye mishahara midogo, huku wenye mishahara mikubwa wakiumia.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, akionyesha mkoba wenye Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, kabla ya kuiwasilisha bungeni, jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM** .

# Vifaa vya ujenzi kutoka nje kodi juu

**Na Salome Kitomari**

KATIKA kujali na kuthamini bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani, serikali imeviongezea kodi vifaa vya ujenzi kutoka nje ya nchi.

Akiwasilisha makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2020/21, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alisema kuwa bidhaa hizo ambazo zitatoka nje zitatozwa ushuru wa forodha.

Bidhaa hizo ni marumaru, misumari, mabati na bidhaa za ujenzi ikiwamo milango na madirisha zitakazoagizwa kutoka nje ya nchi.

Alisema lengo la uamuzi huo ni kuwezesha viwanda vya ndani kuzalisha zaidi na **kuongeza ajira kwa Watanzania.**

**MARUMARU JUU**

Dk. Mpango alisema kuwa bidhaa za marumaru zitaongezewa ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi 35 kwa mwaka mmoja, lengo likiwa ni kulinda na kukuza viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa hiyo pamoja na kuongeza ajira.

**CHUMA**

Alisema serikali itatoza ushuru wa asilimia 10 au Dola za Kimarekani 125 (sawa na Sh. 289.2) kwa kila tani moja ya ujazo kwenye bidhaa za chuma kwa mwaka mmoja kutegemea kiwango.

**MABATI**

Kadhalika serikali imeongeza kodi ya asilimia 25 au Dola za Kimarekani 250 (sawa na Sh. 578.5) kwa kila tani moja ya ujazo kwenye bidhaa za mabati kwa kutegemea kiwango.

Alisema pia serikali imeongeza ushuru wa asilimia 25 au Dola za Kimarekani 200 (sawa na Sh. 462.8), kwa kila tani moja ya ujazo kwa mwaka mmoja lengo likiwa ni kuwalinda wazalishaji wa bidhaa hizo nchini kutokana na ushindani wa nje.

Alisema mabati mengine yatatozwa ushuru wa forodha kwa asilimia 10 yaani Dola za Kimarekani 250 (sawa na Sh. 578.5) kwa kila tani moja ya ujazo kwa mwaka mmoja kutegemea kiwango kipi ni kikubwa kwenye bidhaa za mabati.

"Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani kutokana na udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo zinapoingizwa kutoka nje na kulinda ajira na mapato ya serikali," alisema.

**CHUMA**

Pia serikali itatoza ushuru wa asilimia 25 au Dola za Kimarekani 250 badala ya kiwango cha asilimia 25 au Dola za Kimarekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo kwenye bidhaa za chuma kwa mwaka mmoja kutegemea kiwango kwa mwaka mmoja.

**BIDHAA ZA PLASTIKI**

Alisema itatoza ushuru wa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia ziro kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za fito za plastiki zijulikanazo kama 'PVC Profiles'.

"Bidhaa hizo hutumika kutengenezea fremu za milango, madirisha. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya serikali," alisema.

**KARATASI**

Waziri Mpango alisema serikali itatoza kodi ya asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazozalishwa na kiwanda cha Mufindi.

# Hii ndiyo bajeti ya tano ya JPM

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imewasilisha bungeni makadirio ya bajeti yake kwa mwaka ujao wa fedha, ikionyesha kuwa jumla ya Sh. trilioni 34.88 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho cha miezi 12.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, akiwasilisha bungeni jana hotuba ya makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha itakayokuwa ya tano kwa serikali chini ya Rais John Magufuli, alisema jumla ya mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya halmashauri) yanatarajiwa kuwa Sh. trilioni 24.07, sawa na asilimia 69 ya bajeti yote.

Kati yake, serikali inalenga kukusanya mapato ya kodi ya jumla ya Sh. trilioni 20.33; mapato yasiyo ya kodi ya Sh. trilioni 2.92 na mapato kutoka vyanzo vya halmashauri Sh. bilioni 815.

Serikali pia inatarajia kukopa Sh. trilioni 4.9 kutoka soko la ndani. Kati ya kiasi hicho, Sh. trilioni 3.32 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za serikali zinazoiva na kiasi cha Sh. trilioni 1.59, sawa na asilimia moja ya pato la taifa, ni mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Vilevile, Sh. trilioni 3.04 zinatarajiwa kukopwa kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara kwa lengo la kuongeza kasi katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu.

Alisema washirika wa maendeleo wanatarajia kuchangia misaada na mikopo nafuu yenye jumla ya Sh. trilioni 2.87 ambayo ni asilimia 8.2 ya bajeti.

Kati ya kiasi hicho, miradi ya maendeleo ni Sh. trilioni 2.46; Mifuko ya Pamoja ya Kisekta Sh. bilioni 138.3; na misaada na mikopo nafuu ya kibajeti Sh. bilioni 275.5.

**MATUMIZI**

Alisema serikali inapanga kutumia jumla ya Sh. trilioni 34.88 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, Sh. trilioni 22.1 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 63 ya bajeti na Sh. trilioni 12.78 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Alisema fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zinajumuisha Sh. trilioni 10.48 kwa ajili ya ulipaji wa deni la serikali, Sh. trilioni 7.76 kwa ajili ya mishahara na Sh. trilioni 3.74 kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ambayo yanajumuisha Sh. bilioni 481.9 kwa ajili ya matumizi yatokanayo na vyanzo vya ndani vya halmashauri.

Matumizi ya maendeleo ni Sh. trilioni 12.78. ambayo ni sawa na asilimia 37 ya bajeti yote na yanajumuisha fedha za ndani Sh. trilioni 10.04 na fedha za nje Sh. trilioni 2.74.

Kati ya fedha hizo, Sh. trilioni 2.1 ni kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa reli kwa kiwango cha kisasa; Sh. trilioni 1.6 ni kwa ajili ya mradi wa kufua umeme Mto Rufiji; Sh. bilioni 823.7 ni kwa ajili ya mifuko ya reli, maji na REA; Sh. bilioni 490 ni kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na Sh. bilioni 298.1 kwa ajili ya elimumsingi bila ada.

Pia, alisema serikali imetenga jumla ya Sh. bilioni 600 kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa ya watumishi, watoa huduma na makandarasi wa barabara, maji na umeme.

# Neema wenye mishahara midogo

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imependekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332, ambayo pamoja na mambo mengine, itaongeza makato kwenye mishahara ya waajiriwa.

Vilevile, marekebisho hayo yatakuwa na ahueni kwa waajiriwa wenye mishahara midogo isiyozidi Sh. 270,000 kwa mwezi.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, aliyasema hayo alipowasilisha bungeni jana hotuba ya makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema anapendekeza kufanya marekebisho kwenye sheria hiyo ili kupandisha kiwango cha mapato ya waajiriwa ili kuongeza kiwango cha mapato yasiyotozwa kodi (threshold) kutoka Sh. 170,000 kwa mwezi hadi Sh. 270,000 kwa mwezi (sawa na kutoka Sh. 2,040,000 kwa mwaka hadi Sh. 3,240,000 kwa mwaka) na kubadilisha makundi mengine.

Kwa mujibu wa waziri huyo, waajiriwa walio na mapato ya jumla yanayozidi Sh. 4,320,000 kwa mwaka, lakini hayazidi Sh. 6,480,000 waliokuwa wakitozwa Sh. 205,000 jumlisha asilimia 20 ya kiasi kinachozidi Sh. 4,320,000, sasa watatozwa Sh. 270,000 jumlisha 20 ya kiasi kinachozidi Sh. 6,240,000.

Kwa waajiriwa walio na mapato ya jumla yanayozidi Sh. 6,480,000, lakini hayazidi Sh. 8,640,000, wakitozwa Sh. 637,200 jumlisha asilimia 25 ya kiasi kinachozidi Sh. 4,680,000, sasa watatozwa Sh. 846,000 jumlisha asilimia 25 ya kiasi kinachozidi Sh. 9,120,000.

**KICHEKO KILIMO, MIFUGO**

Waziri huyo pia alisema anapendekeza kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye bima ya kilimo cha mazao. Alisema lengo la hatua hiuyo ni kupunguza gharama na kutoa unafuu katika bima za kilimo, ili kuwawezesha wakulima kuziwekea bima shughuli za kilimo na kuvutia wananchi kutumia huduma za bima kujikinga na majanga mbalimbali yanayoathiri shughuli zao za kilimo, mfano ukame na mafuriko.

Alisema anapendekeza kufanya marekebisho ya kuwawezesha wauzaji wa bidhaa ghafi nje ya nchi kuendelea kujirudishia VAT iliyolipwa kwenye gharama za huduma au bidhaa katika shughuli hizo, ili bidhaa hizo ziweze kushindana katika masoko ya nje.

Waziri huyo pia alisema anapendekeza kuongeza kiwango cha mapato ghafi ya vyama vya ushirika vya msingi yasiyotakiwa kutozwa kodi ya mapato kutoka Sh. milioni 50 hadi Sh. milioni 100 kwa mwaka.

Alisema lengo la hatua hiyo ni kutoa nafuu ya kulipa kodi ya mapato kwa vyama vya ushirika vya msingi zikiwamo SACCOS kutokana na kuwa na mitaji midogo, ili kuwanufaisha wanachama wake kwa njia ya gawiwo na mikopo.

Pia, kufuta msamaha wa kodi ya mapato kwa wazalishaji walio ndani ya maeneo maalum ya kiuchumi (Special Economic Zones)wanaozalisha bidhaa na kuuza ndani ya nchi kwa asilimia 100.

Aidha, alisema katika Sheria ya Usajili wa Magari wamefanya marekebisho kwenye Sheria ya Usajili wa Magari Sura 124, ili kuanzisha usajili wa magari kwa kutumia namba maalum (mfano T. 777 DDD) kwa ada ya Sh. laki tano.

Waziri Mpango alisema uamuzi huo utawawezesha wenye magari kuchagua namba ya usajili wa gari katika namba zilizopo katika regista ya namba za magari katika muda husika.

Alisema hatua hizo za marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Magari inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha Sh. milioni 200.

## Bia, Juisi za ughaibuni ushuru juu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2020/21, itaanza kutoza ushuru kwenye bia za unga (powdered beer), Sh. 844 kwa kilo ya bia ya unga inayoagizwa kutoka nje ya nchi.

Akiwasilisha Bajeti hiyo bungeni jana, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Phillip Mpango, **(pichani)** alisema lengo la mabadiliko hayo ni kupanua wigo wa kodi kwa kuwa bidhaa hizo kwa sasa zinaagizwa kutoka nje ya nchi.

Alisema pia serikali itatoza ushuru wa bidhaa kwenye juisi za unga kwa kiwango cha Sh. 232 kwa kilo ya juisi ya unga inayoagizwa kutoka nje ya nchi.

Waziri Mpango alisema lengo la mabadiliko hayo ni kupanua wigo wa kodi kwa kuwa bidhaa hizo kwa sasa zinaagizwa toka nje ya nchi.

Dk. Mpango alisema kutoza ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa zisizo za petroli kwa ujumla wake zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha Sh. bilioni 45.8.




## Michango ya Covid-19, Ukimwi yaondolewa kodi

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imetangaza kuondoa kodi kwa michango yote inayotolewa na wadau kwenye mfuko wa Ukimwi na Covid-19 katika kipindi cha kuwapo kwa mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alitangaza uamuzi huo jana wakati akiwasilisha makadirio ya bajeti ya mwaka 2020/21 bungeni jijini Dodoma.

Alisema lengo la mabadiliko hayo ni kuhamasisha uchangiaji wa hiari katika Mfuko wa Ukimwi na kwa Serikali ili kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya Ugonjwa wa Ukimwi na COVID 19.

"Napendekeza pia michango iliyotolewa na wananchi kwa serikali na itakayoendelea kutolewa katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya ugonjwa wa Covid- 19 isitozwe kodi hadi hapo serikali itakapotangaza kuisha kwa ugonjwa huu," alisema Waziri Dk. Mpango.

## EFD ushuru chini asilimia 10

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imetangaza kufyeka ushuru wa forodha katika bidhaa mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2020/21, lengo kuu likiwa ni kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi katika sekta mbalimbali.

Akiwasilisha jana bungeni Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alisema mpango marekebisho hayo yametokana na kikao cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki cha Maandalizi ya Bajeti kilichofanyika Mei, 13, mwaka huu kwa njia ya mtandao.

Alisema bajeti ijayo kwenye mashine za kielektroniki zinazotumika kukusanya mapato ya serikali zitapunguziwa ushuru wa forodha kutoka asilimia 10 hadi sifuri.

# Vifungashio korosho, kahawa ushuru sifuri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imepunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia korosho.

Hatua hiyo ilielezwa jana bungeni na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk.Philip Mpango, alipokuwa akiwasilisha mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka 2020/21.

Alisema vifungashio vitakavyohusika ni vile vinavyotambulika katika HS codes 3923.21.00.

"Hatua hii inatarajiwa kuongeza thamani kwenye zao la korosho na kuzipa unafuu wa gharama taasisi zinazohusika na kuchakata korosho hapa nchini, utaratibu wa "Duty Remission" utatumika katika kuagiza vifungashio hivyo,"alisema.

Aidha, alisema pia imepunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia kahawa vinavyotumiwa na viwanda vya kusaga kahawa nchini.

"Vifungashio vitakavyohusika ni vile vinavyotambulika katika HS codes 7310.21.00; 6305.10.00; 3923.50.10; 3923.50.90; 3920.30.90 na 48.19. Hatua hii inalenga kuongeza thamani kwa zao la kahawa na kuvipa unafuu wa gharama viwanda vinavyosaga kahawa hapa nchini,"alisema.

Alisema pia imepunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia pamba.

"Vifungashio vitakavyohusika ni vile vinavyotambulika katika HS codes 3920.30.90; 6305.39.00 na 7217.90.00. Hatua hii inalenga kuvutia uwekezaji ili kuongeza thamani ya zao la pamba nchini,"alisema.

Hata hivyo, alisema kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye magunia yanayoagizwa kutoka nje.

"Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyotengeneza magunia ya mkonge, kukuza na kuendeleza kilimo cha zao la mkonge hapa nchini pamoja na kuongeza ajira na mapato ya Serikali," alisema.

Alisema pia kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mashine za kielektroniki zinazotumika kukusanya mapato ya Serikali (EFD).

# Serikali yaanika athari baa la corona kiuchumi

## Mpango asema kuathiri ukuaji pato la Taifa mwaka 2020

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imelieleza Bunge namna mlipuko wa virusi vya corona ulivyoathiri uchumi wa nchi, kikanda na kimataifa.

Akiwasilisha bungeni jana Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2019 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, kutokana ugonjwa huo kwa mwaka 2020, ukuaji wa pato la taifa unatarajiwa kupungua kutoka matokeo ya awali ya asilimia 6.9 hadi 5.5.

"Ni dhahiri kuwa ugonjwa huu umeathiri uchumi wa nchi nyingi duniani kutokana na vifo, kuongezeka kwa gharama za utoaji huduma katika sekta ya afya na kuathiri shughuli za biashara na uzalishaji hususan kwa nchi zinazotegemea utalii," alisema.

Dk. Mpango alisema serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na ugonjwa huo, akibainisha kuwa hadi sasa, imetoa Sh. bilioni 15.49 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na kinga.

Alisema hatua nyingine ni pamoja na kutolewa msamaha wa kodi kwa aina 15 za vifaa vya kupambana na Covid-19 na kutoa elimu ya jinsi ya kujikinga na maambukizo.

"Jambo jema ni kuwa nchi yetu haikuathirika sana na ugonjwa huu kutokana na hatua madhubuti zilizochukuliwa na serikali chini ya uongozi imara wa Rais Dk. John Magufuli," alisifu.

Alisema kuwa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Aprili mwaka huu, uchumi wa dunia ulikua kwa asilimia 2.9 mwaka 2019 kulinganishwa na asilimia 3.6, mwaka 2018.

Pia, uchumi wa dunia unabashiriwa kuporomoka na kufikia ukuaji wa asilimia hasi tatu mwaka 2020 ambao kwa kiasi kikubwa utachangiwa na athari za mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona.

Alisema katika mwaka 2021, uchumi wa dunia unatarajiwa kuimarika na kufikia ukuaji wa asilimia 5.8 kutokana na matarajio ya kuimarika kwa jitihada za kupambana na ugonjwa huo, ikiwa ni pamoja na kupatikana kwa chanjo na hivyo kutoweka kwa virusi vya corona katika nusu ya pili ya mwaka 2020.

"Matarajio hayo yanatoa mwelekeo wa kuimarika kwa uchumi wa Tanzania na kikanda na hatimaye kuongezeka kwa kipato na kuboresha hali ya maisha ya watu.

Kwa upande wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, alisema kasi ya ukuaji wa uchumi ilipungua kutoka asilimia 3.3, mwaka 2018 hadi asilimia 3.1, mwaka 2019.

Alisema matarajio ya kasi ya ukuaji uchumi utapungua kwa wastani wa asilimia 1.6, mwaka huu kutokana na athari za mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Vilevile, alisema katika ukanda huo, uchumi unatarajiwa kuimarika na kufikia wastani wa asilimia 4.1, mwaka 2021 kutokana na jitihada za kupambana na ugonjwa huo.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, akiwasilisha taarifa ya hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2019 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

Alisema yapo matarajio ya kuongezeka kwa misaada kutoka nchi zilizoendelea kwa ajili ya kupambana na ugonjwa huo na matarajio ya utulivu wa bei ya nishati ya mafuta katika soko la dunia.

Alisema uchumi wa nchi za ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliendelea kuimarika na Tanzania ilikuwa na ukuaji wa asilimia saba, Rwanda asilimia 9.4, Uganda asilimia 4.9 na Kenya asilimia 5.4.

"Kutokana na athari za Covid-19, ukuaji wa uchumi wa ukanda huo unatarajiwa kupungua kwa mwaka 2020 na hatimaye kuanza kuimarika mwaka 2021 kutokana na juhudi zinazochukuliwa na nchi wanachama katika kupambana na athari za ugonjwa huo, zikiwamo za kifedha na kibajeti pamoja na utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo katika sekta za uchukuzi (reli, barabara na madaraja) maji, nishati, elimu na afya," alisema.

**SEKTA VINARA**

Dk. Mpango alibainisha kuwa mwaka 2019, pato la taifa lilikua kwa asilimia saba kama ilivyokuwa mwaka 2018 na kuwa ukuaji huo ulitokana na uwekezaji hususan katika miundombinu ikiwamo: Ujenzi wa barabara, reli na viwanja vya ndege; kutengamaa kwa upatikanaji wa nishati ya umeme; kuimarika kwa huduma za usafirishaji; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini hususan dhahabu na makaa ya mawe; na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Kwa mujibu wa Dk. Mpango, sekta zilizokua kwa viwango vikubwa kwa kipindi hicho ni pamoja na uchimbaji madini na mawe (asilimia 17.7); ujenzi asilimia 14.8; sanaa na burudani asilimia 11.2; na usafirishaji na uhifadhi mizigo asilimia 8.7.

**DENI LA SERIKALI**

Dk. Mpango alibainisha kuwa hadi Aprili mwaka huu, deni la serikali lilifika Sh. trilioni 55.43. Kati ya kiasi hicho, deni la nje lilikuwa Sh. trilioni 40.57 na deni la ndani Sh. trilioni 14.85.

"Deni la serikali lilichangiwa na kupokewa kwa mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi.

"Matokeo ya tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Desemba 2019, yameonyesha kuwa deni la serikali ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu," alisema.

Aliyataja mafanikio 17 ya serikali ya awamu ya tano kuwa ni pamoja na ukuaji wa uchumi kwa wastani wa asilimia 6.9; ujenzi wa reli ya kisasa (SGR); mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere; utekelezaji wa mradi wa REA; kuboresha Shirika la Ndege kwa kununua ndege mpya 11; na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege.

Mengine ni ujenzi na ukarabati wa bandari; ujenzi na ukarabati wa meli katika maziwa makuu; ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja; Kanda Maalum za Kiuchumi; kuimarisha sekta za kilimo, mifugo na uvuvi; kuhamia Dodoma; utekelezaji wa miradi ya sekta ya afya; utekelezaji wa miradi ya elimu; miradi ya maji mijini na vijijini; marekebisho katika mikataba na sheria za madini; na uendelezaji wa viwanda.

**VIPAUMBELE**

Alisema mwaka huu nchi imepata mvua kubwa iliyosababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu, hivyo katika mwaka 2020/21, serikali itaweka kipaumbele katika ukarabati wa miundombinu ya kiuchumi na kijamii iliyoharibiwa na mvua ikijumuisha barabara na madaraja, reli, nguzo za umeme, mabwawa ya maji na majengo ya taasisi za afya na elimu.

Waziri huyo alivitaja vipaumbele vingine kuwa ni viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda; kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu hasa kwenye sekta za maji, elimu na afya; uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji; na kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa mpango wa maendeleo.

# Madereva waliokwama mpakani wahaha

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

MKUU wa Wilaya ya Longido mkoani Arusha, Frank Mwaisumbe, amewataka wamiliki wa malori yanayopeleka mizigo nchi jirani ya Kenya kutafuta ufumbuzi wa maisha ya madereva wao waliokwama mpaka wa Namanga.

Kwa mujibu wa Mwaisumbe, madereva wanaonekana kuwa ombaomba kutokana na kushindwa kumudu gharama za kujikimu katika kipindi hiki ambacho mwingiliano wa kibiashara baina ya nchi hizo unatishiwa na virusi vya corona.

Akizungumza jana na wasafirishaji jijini Arusha, alisema kuwa serikali haiwezi kukubaliana na hali hiyo ya madereva kuteseka kwa kukosa fedha za kujikimu huku akitaka kubaini tatizo linalosababisha mateso kwa madereva hao.

Mwaisumbe alisema robo tatu ya madereva waliokwama katika mpaka huo upande wa Tanzania hali zao ni mbaya na kuwaagiza wamiliki wa malori hayo kufika na kujionea mazingira hayo, ili kutafuta ufumbuzi kwa kushirikiana na viongozi wa serikali.

"Suala kubwa lililopo ni kuendelea kuwasiliana na viongozi na mabalozi pande zote mbili ikiwamo Tanzania na Kenya," alisema Mwaisumbe.

Aliagiza wanaojishughulisha na kutoza ushuru wa maegesho ya magari mpakani, kutoza siku ya kwanza gari linapoingia kwenye eneo la egesho na linapoendelea kukaa mpakani lisitozwe kwa kuwa biashara yake imesimama.

Mwakilishi wa Chama cha Malori Kanda ya Kaskazini, Zainabu Athumani, amesema kutokana na mikataba, madereva wengi wamepewa pesa zinazotosheleza licha ya baadhi yao kutowatosha.

Pia ameomba wakati suala hilo likingoja ufumbuzi, magari ya Tanzania yaliyo na mizigo ya kwenda Kenya yaruhusiwe kushusha mizigo na kurudi ili kuepuka baadhi ya bidhaa kuharibika na kupata hasara kwa kuwa vita hiyo siyo ya corona ni ya kiuchumi.

"Tunaona vita hii ni ya kiuchumi na si ya corona, kama inavyodaiwa," alidai Zainabu.

Alisema kuna gari limekwama mpakani hapo ambalo limepakia kontena ya baruti jambo ambalo ni hatari na msafirishaji wa mzigo huo anajuta kutokana na hasara iliyojitokeza ambayo kwa sasa inakadiriwa zaidi ya Dola za Marekani 1000.

Baadhi ya madereva waliokwama kwenye mpaka huo, walikiri kukosa fedha za kujikimu na huku wakilalamikia wamiliki wa magari hayo kutopokea simu zao na wakati mwingine wakipokea hawana majibu ya kuridhisha.

Yusuph Hassan, alidai kukwama mpakani hapo kwa wiki mbili na kilichosababisha ni baada ya uongozi wa Kenya kukataa vyeti vya vipimo vya virusi vya corona vya upande wa Tanzania na kutaka kuwapima mara ya pili.

Samson Mathias, alisema kwa wiki ya pili sasa mmiliki wa gari amemtumia Sh. 20,000 na kusababisha wakati mwingine kulala njaa au kula mlo mmoja kwa siku. Wameiomba serikali kuingilia kati na kutatua hali hiyo.

# Makonda atoa neno hoteli kurudi baada ya corona

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amesema kitendo cha kufunguliwa kwa hoteli ya Hyatt Regency maarufu kwa jina la Kilimanjaro itasaidia kuongeza uchumi kwa Jiji la Dar es Salaam.

Hoteli hiyo ilifungwa kwa kuhofia mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona mwishoni mwa mwaka jana.

Makonda ameyasema hayo jana jijini wakati akizungumza na waandishi wa habari alipokwenda katika hoteli hiyo kushuhudia kufunguliwa na jinsi ilivyojiwekea utaratibu wa kukabiliana na maambukizo ya virusi hivyo.

"Naomba niwapongeze wamiliki wa hoteli na watumishi wote kwa kurejea kutoa huduma, sote tunafahamu hii ni miongoni mwa hoteli kubwa.

Na tayari tumesharuhusu kufungua anga letu na kupokea ndege za kimataifa, watalii wetu watafika katika hoteli hii na kuongeza uchumi pamoja na watu wengine," alisema Makonda.

Makonda alisema hoteli hiyo ipo vizuri kiusalama kwani ameikagua na kuona jinsi walivyoweka tahadhari ya kutosha kuepisha maambukizo, ikiwamo kuweka vitakasa mikono kila sehemu na kutoa barakoa.

"Nimefurahi hata utaratibu wa menu (vyakula) umebadilika, unachukua simu yako na 'kuskani' unapata aina ya vyakula unavyovitaka na kuagiza... hii ni hatua kubwa iliyochukuliwa katika kujilinda na kuzuia ugonjwa wa corona."

Makonda aliuomba uongozi wa hoteli punguzo la bei za huduma zake hususani kwa Watanzania na hasa wakazi wa Dar es Salaam ili katika kipindi hiki cha mapambano na ugonjwa huo yanazidi kupungua.

Aidha, Makonda alisema hofu zilizosambazwa kuwa mkoa huo haupo salama, sio la kweli.

Alisema sio muda mrefu atamwomba kiongozi mmoja wapo wa kitaifa kutembelea hospitali ambazo zinazushiwa kuwa na wagonjwa wengi wenye corona

Meneja Masoko wa Hoteli hiyo, Lilian Kisasa, alimpongeza Makonda kwa kufanya uzinduzi huo na kumhakikishia kuwa uongozi umejipanga kutoa huduma zake bora kama ilivyokuwa awali.

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

## TAARIFA KWA WAFANYABIASHARA

## AGIZO LA KUUZA MAFUTA

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetoa leseni zaidi ya 1,600 za kuendesha vituo vya mafuta katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuhakikisha mafuta yanapatikana kwa urahisi na usalama. Kwa mujibu na masharti ya leseni hizo, vituo vya mafuta vinapaswa kufanya biashara ya mafuta kila siku.

Hata hivyo, katika siku za hivi karibuni, EWURA imebaini kuwepo kwa vituo vya mafuta ambavyo havifanyi biashara kwa maelezo ya kukosa mafuta kutoka kwa wauza mafuta kwa jumla. EWURA inawafahamisha wamiliki wote wa vituo vya mafuta kuwa, maghala ya mafuta yana hifadhi ya kukidhi mahitaji ya nchi kwa zaidi ya mwezi mmoja. Hivyo basi, hakuna kituo kitakachoshindwa kufanya biashara kwa sababu ya uhaba wa mafuta. Iwapo kituo chochote hakitauziwa mafuta na wafanyabiashara wa jumla, kitoe taarifa EWURA iliyoambatishwa na uthibitisho wa kutouziwa mafuta.

Aidha, ili kuhakikisha biashara ya mafuta inakuwa endelevu katika maeneo yote nchini, **kila kituo cha mafuta kinatakiwa kuwa na mkataba au mikataba** na wafanyabiashara wa jumla ya kununua kiwango cha mafuta cha kukidhi mahitaji ya eneo husika kulingana na uwiano wa soko la mafuta la kituo husika.

Vilevile, wakati wa kuagiza mafuta (order) kutoka kwa wafanyabiashara wa jumla, **kila kituo kitatakiwa kuagiza au kuweka *order* hiyo kwa maandishi** na kuhifadhi nyaraka zote kwa ajili ya ukaguzi wa EWURA. Mfumo wa maandishi unaoweza kutumika ni pamoja na barua pepe au nukushi.

**Hivyo basi, EWURA inatoa AGIZO kwa vituo vyote vya mafuta kuhakikisha vinakuwa na mafuta ya kukidhi mahitaji ya maeneo yao ya biashara kulingana na *umiliki* wa s*oko wa kituo husika.***

Iwapo kituo chochote cha mafuta kitashindwa kufanya biashara ya mafuta, EWURA itachukua hatua za kisheria kwa k**ituo husika na wauzaji wa jumla watakaothibitika kutouza mafuta kwa kituo husika.** Adhabu hiyo itakuwa ni pamoja na kufuta leseni kulingana na kifungu cha 143 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392.

**Mhandisi Godfrey Chibulunje**
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**
**10 Juni 2020**

215770302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bajeti yetu ya Tanzania ya viwanda

**MIAKA** mitano inamalizika na bajeti ya mwisho ya taifa ya mwaka 2020/21 imewasilishwa bungeni jana. Bajeti ya serikali imefunga awamu ya kwanza ya miaka mitano ya serikali iliyoanza kazi mwishoni mwa mwaka 2015.

Kwa ujumla mambo mengi yamefanyika kwa miaka mitano na tunaipongeza serikali kwa kujitahidi. Kikubwa zaidi ni kutumia jitihada zote kuifanya Tanzania kuwa taifa linalojitegemea kiuchumi.

Jitihada zimefanyika ikiwa ni pamoja na kuanzisha viwanda vya kuzalisha vifaa vya ujenzi kama vigae, marumaru na taasisi za umma kama mifuko ya hifadhi ya jamii kuanzisha viwanda.

Hata hivyo, tunaikumbusha serikali kuwa taifa linahitaji sana viwanda ili kufikia azma ya Tanzania ya viwanda. Hata hivyo azma hiyo bado ina changamoto nyingi na haijakamilika.

Tunaamini kuwa kitakachotuondolea umaskini na kutuwezesha kuwa na nguvu kiuchumi ni kuwa na viwanda ambavyo tutaajiri watu wetu, tutazalisha na kupata fedha za kigeni na kutumia malighafi zetu ambazo nyingi tunaziuza ghafi ughaibuni.

Ndiyo maana serikali inaposoma na bunge kupitia bajeti ya mwisho katika muhula wa miaka mitano tunaikumbusha serikali kuwa taifa linaendelea kuhitaji kuiona mipango madhubutu ya kufanya Tanzania ya viwanda.

Tunasisitiza kuwa viwanda ni muhimu kutokana na ukweli kuwa ukosefu wa sukari uliolisumbua taifa kwa karibu miezi miwili unaonyesha kuwa kuna haja ya kuwekeza zaidi kwenye sekta ya viwanda.

Ni vyema serikali ikumbuke kuwa baadhi ya viwanda vilikuwa vinafanyakazi, lakini vikabinafsishwa na kilichotokea si kuviendeleza bali ni kuvimalizia. Ukweli ni kwamba kwa sasa vingi vimeng'olewa mitambo yote, vitasa na cha kushangaza hata masinki na bomba za vyooni.

Ushahidi upo kwenye kiwanda cha Tanganyika Packers cha Dar es Salaam kilichokuwa kinasindika nyama leo kimebaki gofu la kuta zilizopasuka.

Viwanda vingine vimegeuzwa maghala au magodauni ni kwanini wanunuzi wanafanya hivyo? Watanzania wanahitaji majibu ikiwezekana taarifa zitolewe bungeni na mikakati inayoendelea ya kufufua viwanda hivyo kwani bila viwanda mambo ni magumu.

Lakini, pia ubinafsishaji wa viwanda bado umeshindwa kuendeleza sekta hiyo badala yake tunaona vingi vikigeuzwa magofu na maghala ya kukodishwa ama kwa wawekezaji kutoka nje au kampuni za humu nchini.

Kuna baadhi ya viwanda vilibinafsishwa katika utaratibu wa serikali kugawana hisa na mwekezaji.

Mfano, baadhi ya viwanda vya nguo, lakini ubinafsishaji wake haujafanya maboresho na kuviimarisha ili vizalishe kisasa na kuongeza tija.

Ubinafsishaji katika maeneo hayo huenda haujaleta mtaji, teknolojia ya kisasa wala uwezo wa kujiendesha kwa viwanda hivyo badala yake ni kupata hasara kila siku.

Kwa msingi huo bunge linavyomaliza muda wake na bajeti yake ya mwisho kuwasilishwa bungeni tayari kwa kujadiliwa na kupitishwa kuna haja ya serikali kuanza kuchakata upya namna ya kufikia malengo ya Tanzania ya viwanda.

Ni wazi kuwa bila viwanda hatuwezi kuajiri Watanzania, kupata fedha za kigeni, kuondoa umaskini na pia kutumia rasilimali zilizoko kwa ajili ya viwanda na uzalishaji wa bidhaa za ndani.


Tunaishauri serikali kuanza kuchunguza tena suala la viwanda kwani huenda azma hii itahitaji nguvu na msukumo mpya.

Kama taifa hutuwezi kutegemea mafanikio kama hatutajizatiti kujenga viwanda na kuwa wazalishaji wa bidhaa zetu wenyewe.

Wakati bunge linaendelea kujadili bajeti ya 2020/21 tunaishauri serikali kuangalia namna bora ya kuchakata bidhaa zetu wenyewe kwa kujenga viwanda ili juhudi zinazochukuliwa kama kujenga miundo ya maji, usafirishaji na nishati zinufaishe taifa letu kikamilifu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Nanenane karibu, ila jamani yawafuate wakulima waliko



Na Sabato Kasika

KWA mara ya tatu mfululizo, Maonyesho ya Kilimo na sherehe za Nanenane kitaifa kwa mwaka 2020 yatafanyika katika viwanja vya Nyakabindi, Bariadi mkoani Simiyu.

Viongozi wa kitaifa wanatarajia kushiriki katika maonyesho hayo, kama alivyotamka Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka.

Kama ilivyo utamaduni, washiriki wa Nanenane kitaifa Simiyu hawakosi watu binafsi, taasisi mashirika ya umma na wadau wa kilimo, mifugo na uvuvi, wanaohimizwa kuanza maandalizi mapema.

Utaratibu wa sherehe hizo, ni muhimu uchochee kwa kiwango kikubwa kuwafanya wahusika kuzingatia mbinu mbalimbali za kuboresha shughuli za kilimo na ufugaji nchini.

Mfano mmojawapo, ni kwamba wakulima wamekuwa wakipewa elimu mbalimbali ya kuboresha kilimo, hivyo ni wajibu wa wahusika kupokea na kutumia mbinu hizo kwenye shughuli zao.

Wakifanya hivyo, watanufaika na maonyesho hayo, ingawa inawezekana kuwapo changamoto za hapa na pale, lakini kimsingi, kuzingatia elimu ya kilimo na ufugaji bora ni muhimu.

Hivyo, maonyesho yanapofanyika kwenye kanda mbalimbali, yanatoa fursa kwa serikali kuona ni mahali pa kuongeza nguvu ya matumizi ya teknolojia, kuendeleza mazao au mifuko na uvuvi kwa kanda husika.

Maana yake ni kwamba, lengo kubwa ni Watanzania wadau wa kilimo, ufugaji na uvuvi, wanufaike na kile wanachokifanya na kulipa kodi kwa maendeleo ya taifa na watu wake.

Ikumbukwe, maonyesho hayo kitaifa hufanyika mkoa mmoja hadi mwingine na walengwa wa kila mkoa hawana budi kushiriki na kujitangaza kupitia fursa za kuboresha shughuli zao.

Kikubwa zaidi, ni wahusika wasishiriki maonyesho kwa mazoea pekee, bali kila wanaposhiriki watoke na kitu kipya walichojifunza kwa ajili ya kuboresha shughuli zao za kila siku za uzalishaji mali. Hilo unaenda hadi ujumbe wa taarifa mbalimbali za mawasiliano kutoka maonyesho.

Wataalamu wa fani mbalimbali huwa washiriki katika maonyesho hayo ili kutoa elimu, kwa hiyo awe mkulima, mfugaji au mvivu, ni lazima atatoka na kitu alichojifunza, iwapo atazingatia elimu ya wataalamu hao.

Ninaamini kwamba wakulima huwa wanafundishwa jinsi ya kuandaa mbegu, kupanda, kutunza shamba, kuvuna, kutafuta masoko, kuyapa thamani mazao ya kuleta maendeleo kwa ajili ya kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla.

Vivyo hivyo, hata wafugaji na wavuvi nao kwa upande wao hufundishwa jinsi ya kuboresha ufugaji na uvuvi. Kwa hiyo, msisitizo mkuu uko kwenye kuzingatia elimu inayotolewa na wataalamu.

Kwa kuzingatia utaalamu, wahusika wanaweza kunufaika na kuwa wakulima, wafugaji na wavuvi wakubwa, pia ni vyema nikatoa angalizo kuhusu maonyesho hayo.

Hapo kuna suala la uhakikisha maonyesho hayo yaelekezwa kwenye maeneo ya wahusika zaidi, badala ya kujikita mijini kama yale ya viwanja vya Nanenane mjini Morogoro.

Kufanya maonyesho kama hayo maeneo ya mijini, yawezeza kuwafanya wakulima wakashindwa kumudu gharama za kuwafikisha huko, hivyo ni muhimu sasa au huko tuendako lifanyiwe.

Hivyo, ni muhimu kuhamisha maonyesho yakapelekwa kwa wakulima wadogo kule vijijini, ili waweze kushiriki kikamilifu, badala ya kuyaweka mijini na kuwaacha mbali walengwa.

Ni bahati nzuri mkoa wa Simiyu umeliona hilo na kwa miaka miwili mfululizo, maonyesho yamekuwa yakifanyika kitaifa kwenye viwanja vya Nyakamindi ambako ni mbali na mjini na sasa wanajiandaa kufanya kwa mara ya tatu.

Ni maoni yangu, bado kuna changamoto kubwa inayohitaji kufanyiwa kazi na wahusika, ili Nanenane iweze kuleta manufaa kwa wakulima wakubwa na wadogo.

Mojawapo ni kuhamisha maonyesho na kupelekwa kwa wakulima wadogo vijijini, ili waweze kushiriki kikamilifu badala ya kuyaweka pembezoni mwa miji mikuu na kuwaacha mbali wakiwa hawana uwezo wa kufika mijini.

Nina uhakika hata yakifanyika vijijini itakuwa ni rahisi kwa wakulima wakubwa kufika huko bila tatizo.

Lakini kwa utaratibu wa sasa sidhani kwamba wakulima wadogo wananufaika kulingana na hali halisi ya maisha yao kule waliko.

Nimalize kwa kukumbusha kilio changu, asilimia kubwa ya Watanzania wanategemea kilimo na wanaishi vijijini, huku maonyesho yanakuwa mbali na waliko.

# ‘Wafanyabiashara msiwakimbie TRA’

Na Oliver Njunwa

WAFANYABIASHARA jijini Dar es Salaam wameshauriwa kutowakimbia maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), wanapowatembelea katika maeneo yao ya biashara na kutakiwa kutoa ushirikiano ili waweze kufaidi elimu na ushauri unaotolewa na maofisa hao.

Ushauri huo ulitolewa na baadhi ya wafanyabiashara wa Tabata Segerea, ambao walipata fursa ya kupatiwa elimu wakati wa kuelimisha wafanyabiashara katika maeneo yao ya kazi, huku wengine wakifunga maduka yao.

“Nimepata mafunzo mazuri baada ya kuwapatia maelezo ya biashara yangu na upungufu nilionao. Wamenielimisha vizuri na kunishauri mambo mazuri kuhusu biashara yangu,” alisema Jamila Mgeni mfanyabiashara wa nguo Tabata Segerea na kuongeza: Mfanyabiashara hana sababu ya kufunga duka au kusingizia kwamba mwenye duka hayupo kwa kuwa kufanya hivyo ni kupoteza nafasi ya kuelimishwa.”

Jamila alisema endapo mfanyabiashara ana changamoto katika makadirio ya kodi ni vyema akakubali kutembelewa na maofisa wa TRA ili wamsaidie na kumwelekeza cha kufanya.

Katika hatua nyingine mfanyabiashara huyo aliwasihi wafanyabiashara kulipa kodi kwa wakati ili shughuli ambazo zinafanywa na serikali za kijamii na kiuchumi ziweze kutekelezwa kwa ukamilifu.

Babin Mohammed, mfanyabiashara wa nguo za mtumba alisema kuwakimbia maofisa wa TRA hakuna faida na kwamba wanaokimbia inawezekana kuna makosa wanayoyafanya au wana upungufu, hivyo ni vyema wakubali kuwasikiliza ili waweze kusaidiwa kwa kuelimishwa na kupatiwa ushauri wa kutatua changamoto zinazowakabili.

Aliema yeye kuna vitu alikuwa anafanya kimakosa, lakini hawakumkaripia bali walimwelewesha kwa utaratibu na kuahidi kufuata ushauri wao.

Akizungumzia wafanyabiashara kutembelewa maeneo yao ya biashara, Ofisa Msimamizi wa Kodi, Lameck Ndinda, alisema amesikitishwa na wafanyabiashara ambao wanafunga maduka yao na kuwashauri kutoa ushirikiano ili lengo la elimu liweze kufanikiwa.

“Lengo la zoezi hili ni kuwaelimisha wafanyabiashara, kufahamu changamoto zinazowakabili, na kupata maoni yao na ushauri kuhusu huduma zinazotolewa na TRA,” alisema Ndinda.

Alisema uamuzi wa kuwatembelea wafanyabiashara pia ni kuwahamasisha kulipa kodi kwa wakati ili kuwaepusha na adhabu zinazotokana na kulipa kodi kwa kuchelewa.


## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

## CHUO CHA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVUKAZI (ATTI – MBEYA)

## TANGAZO LA KOZI ZA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI (LBT)

**1. Utangulizi:**

Chuo cha Mafunzo ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi “Appropriate Technology Training Institute” (ATTI- MBEYA) ni Chuo cha Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kinawatangazia wananchi wote kuwa kinatarajia kuanza kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo/Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. Kozi hizi zimepangwa kufanyika kama ifuatavyo: -

| Na. | JINA LA KOZI | MUDA NA TAREHE | MAFUNZO YATAFANYIKA |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi ya uwekaji wa tabaka la Lami kwenye barabara za miji na vijiji (‘Bituminous surfacing of low traffic volume roads’) kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | Wiki Nne (4) 14/09/2020 - 09/10/2020 | ATTI – Mbeya |
| 2 | Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | Wiki Kumi (10) 12/10/2020 - 18/12/2020 | ATTI- Mbeya |
| 3 | Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi (Kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana). | Wiki Nne (4) 23/11/2020 - 18/12/2020 | ATTI – Mbeya |

**2. Masomo Yatakayofundishwa: -**

(a) **Kozi ya Mafunzo ya Matengenezo na Ukarabati wa Barabara za Lami:** Washiriki watajifunza aina za lami, aina za barabara za lami, aina za viunzi vya ujenzi wa barabara za lami (‘Bituminous road construction materials’); aina ya Vifaa na mitambo kwa kazi za ujenzi wa barabara katika kiwango cha lami; kusanifu na kutengeneza tabaka la lami ‘Design and construction of Surface Dressing’; kuziba viraka; kuziba mipasuko ‘crack sealing’; na Usalama kazini. Lengo kuu la kozi hii ni kumwezesha mshiriki kupata ujuzi wa kusanifu (design) na kufanya kazi za ukarabati na matengenezo ya barabara za lami “Surface Dressing”.

(b) **Kozi ya Mafunzo ya Matengenezo na Ukarabati wa Barabara za Udongo/Changarawe:** Washiriki watajifunza mada mbalimbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. Aidha, watajifunza juu ya; mpango wa kazi (Planning), Uongozi sehemu za kazi na mbinu za usimamiaji wa kazi, vipimo vya kazi, usimamiaji wa mikataba, Uwekaji wa changarawe pamoja na ujenzi wa makalavati. Kozi hii imekusudia kumwezesha mshiriki kupata ujuzi wa kutosha katika kufanya na kusimamia kazi za ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe/udongo kwa ubora unaotakiwa.

(c) **Kozi Maalumu ya Vikundi vya Wanawake na Vijana:** Washiriki watajifunza mada mbali mbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na masomo shirikishi ambayo ni utaratibu wa kufungua kampuni kwa vikundi, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, uashi, teknolojia ya udongo na zege. Kozi hii imelenga kumwezesha mshiriki kupata ujuzi wa kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hususani matengenezo ya kawaida yaani ‘Routine/Recurrent maintenance’.

**3. Njia za Ufundishaji**

Mafunzo haya yatahusisha mafunzo kwa nadhalia na vitendo.

**4. Malengo ya Kozi**

Kozi hizi zimelenga kumpatia mshiriki mbinu za matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi katika:

i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani ‘Routine/Recurrent, Periodic and Emergency maintenance’;
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani ‘road rehabilitation’;
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara;
iv. Kuwezesha wajasiriamali, kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani “SPECIALIST LABOUR BASED CONTRACTING FIRMS” kisha kupata sifa za kisheria za kuomba miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara inayotolewa na wakala wa Barabara na sekta binafsi.

**5. Walengwa wa Mafunzo haya ni: -**

a) Wahandisi wote wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi, b) Mafundi Sanifu wa Barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
c) Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi nchini,
d) Makandarasi wenye nia ya kujenga uwezo wa kazi zao za matengenezo ya barabara kwa kutumia Tekinolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
e) Watu binafsi wenye uzoefu wa kazi za barabara na wanaotaka kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**6. Lugha ya mafunzo: -**

Kozi zote zitaendeshwa kwa kutumia lugha ya kiingereza isipokuwa kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana ambayo itaendeshwa kwa mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

**7. Gharama za Mafunzo: -**

Gharama za mafunzo ni **Tshs. 1,000,000/=** Kwa kozi ya Matengenezo na Ukarabati wa Barabara za Lami, **Tshs. 1,600,000/=** Kwa kozi ya Matengenezo na Ukarabati wa Barabara za Udongo/Changarawe na **Tshs. 500,000/=**
Kwa kozi Maalumu ya Vikundi vya Wanawake na Vijana.

**8. Malipo: -**

Malipo ya ushiriki yalipwe kabla ya kozi kuanza kupitia Tawi lolote la Benki ya **NBC;** Control Namba ya malipo wasiliana nasi kwa Simu: - 0766581616/0763651034. NB: Malipo yalipwe kabla ya wiki mbili na hati ya malipo iwasilishwe ufikapo Chuoni ATTI - MBEYA.

**9. Namna ya Kutuma Maombi ya Kozi hizi: -**

Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi hizi wanaombwa kutuma maombi yao Chuoni ATTI – MBEYA kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizowekwa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa maelezo zaidi.

**Kumbuka:** Nafasi zilizopo ni ishirini (20) tu kwa kila kozi hivyo, tuma maombi yako mapema. Aidha, washiriki wote ambao wameshalipia ada wafike Chuoni kwa tarehe zilizoonyeshwa watakaochelewa kufika hawatapokelewa.

**Wasiliana nasi Kupitia:**
**MKUU WA CHUO, ATTI – MBEYA, S.L.P 1957, MBEYA.**
**Simu: 025 295 7484/5; 0787 059 555; 0769 317 404; 0765 251 509**
**Nukushi: 025 295 7486, Barua pepe: attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com**

21771702

# JPM amsamehe Kamishna Andengenye

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS John Magufuli amemsamehe aliyekuwa Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengenye na maofisa wengine wa jeshi hilo waliotuhumiwa kusaini mkataba tata wa Sh. trilioni 1.04 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya jeshi hilo.

Kauli hiyo aliitoa jijini hapa jana alipokuwa akizindua jengo la makao makuu ya jeshi hilo, ambalo ujenzi wake umegharimu kiasi cha Sh. bilioni 2.65 lililojengwa kwa mfumo wa Force Account.

Alisema pamoja na msamaha huo kamishna huyo hatamrudisha kwenye jeshi hilo, lakini anamtafutia kazi nyingine.

"Yaliyopita si ndwele tugange yajayo, lakini yasijirudie, sasa tuanze kuganga mapya tuchape kazi makamanda wa jeshi hili najua mmepitia changamoto nyingi hasa kwenye mradi wa ajabu uliofanywa na kamishna niliyemtoa," alisema.

Alishukuru jeshi hilo kufanya marekebisho, na kwamba kulikuwa na mapendekezo ya kwamba makamishna wanne washushwe vyeo na wengine awafukuze.

"Nataka niwaambie nimeangalia kwanza mnavyopendeza, nikawaangalia mlivyo na huruma na upendo mkubwa wa kufanya kazi na nyuso zenu mnaonyesha hivyo kwa hiyo nimewasamehe," alisema.

Aliongeza: "Kwa hiyo Simwanza wewe ulikuwa unaondoka na wengine sitaki kuwataja majina nimewasamehe, lakini nafanya haya kwa unyenyekevu mkubwa sana na kwa kumwogopa Mungu... sisi wote ni wadhambi unapomwona mtu anaonyesha dalili za ku regret 'kujitia' msamaha lazima utoke."

Alifafanua kuwa fedha za bure katika kipindi cha utawala wake ni mbaya na zitawaharibia maisha yao, na kwamba hata waroge kiasi gani yeye habadiliki kwa sababu anataka fedha hizo za walipakodi zikalete matokeo na thamani ya fedha ionekane.

"Makamanda wote ni wazuri, hakuna wabaya tukachape kazi na mimi mtumishi wenu ninawapenda mno tofauti na mnavyofikiria nawathamini na nasema hili kwa dhati," alisema.

Alisema Kamshina Andengenye alimwomba msamaha zaidi ya mara tatu, na sasa ameamua kumsamehe kwa kuwa ameonesha kukiri kosa lake na anahitaji msamaha.

"Mungu awasamehe na mimi najua mmebadilika kweli kweli mkikutana na Andengenye mwambieni nimemsamehe ameomba msamaha karibu mara tatu amekiri kweli kweli, lakini kwenye jeshi hili hatarudi mtamwona sehemu nyingine kwa hiyo uliyepo usiogope kwamba utatolewa," alisema.

Aliongeza: "Msamaha niliotoa ndio umenifanya nifurahi maana ukibaki na kitu moyoni maana yake hujasamehe nimewasamehe wote, hivyo yaliyopita si ndwele tugange yajayo nendeni mkachape kazi," alisisitiza.

Alipongeza jeshi hilo kwa utendaji kazi wake na kuahidi kutoa kiasi cha Sh. bilioni tano kwa ajili ya kujenga makazi ya askari wa jeshi hilo ndani ya wiki moja kuanzia sasa.

Aliahidi kuendelea kutatua changamoto zao kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana, huku akimtaka Kamshina Jenerali Masunga kusikiliza shida na kero za watumishi wake na kutafuta mbinu za kutatua.

Aliagiza viongozi wa Manispaa, Majiji na Wizara ya Ardhi, kuelimisha wananchi juu ya kuacha njia kwa ajili ya magari ya kuzimia moto kupita.

Awali, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alisema ujenzi wa jengo hilo umetumia utaratibu wa force account kama ambavyo Rais alielekeza na imesaidia jengo kukamilika ndani ya muda mfupi na kutumia gharama ndogo ikilinganisha na mwonekano wake.

Naye, Kamshina Jenerali wa jeshi hilo, John Masunga, alibainisha changamoto zinazowakabili ikiwamo ukosefu wa makazi kwa ajili ya askari na nyumba zinazohitajika nchi nzima ni 2,457 na zilizopo ni 49 tu.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2019/20 jeshi linatarajia kukamilisha ununuzi wa magari matano mapya yatakayogharimu Sh. bilioni 3.7 kutoka Shirika la Nyumbu.

Machi 13 mwaka huu, Serikali ya Tanzania ilivunja mkataba tata uliosainiwa baina yake na kampuni ya ROM Solutions ya Romania ambao ulikua unahusu ununuzi wa vifaa vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa gharama ya Euro 408,416,288.16 ambazo ni sawa Sh. trilioni moja za Kitanzania.

Mkataba huo uliingiwa Agosti 22, 2019 na ulisababisha kutumbuliwa kwa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola na Andengenye.



Rais John Magufuli, akizungumza na watumishi mbalimbali wa serikali kabla ya kufungua jengo la ofisi za makao makuu ya Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura), jijini Dodoma, jana. **PICHA: IKULU**.

# Stendi ya Mbezi rasmi mwaka huu

**Mary Geofrey na Fatma Mtutuma (UDOM)**

UJENZI wa kituo cha mabasi ya mkoani Mbezi Mwisho jijini Dar es Salaam, umefika asilimia 79 na unatarajia kukamilika mwaka huu.

Kaimu Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Abdallah Mtinika, aliyaeleza hayo wakati akipokea msaada wa mashine saba za kunawia mikono na sabuni lita 720 kutoka Shirika la WaterAid.

Misaada hiyo imekabidhiwa kwa ajili ya kutumiwa katika kituo cha mabasi Ubungo, kituo kikuu cha mabasi yaendayo haraka Gerezani na Kimara Mwisho kwa ajili ya matumizi ya abiria wanaoingia na kutoka katika vituo hivyo.

Mtinika alisema kituo hicho ni cha kisasa ambacho kitakuwa na mahitaji yote na kwamba serikali ilitoa Sh. bilioni 51 kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya ujenzi wake.

Kadhalika, alisema kituo hicho kina uwezo wa kuingiza mabasi 700, magari madogo 80 na nje kutakuwa na eneo lenye uwezo wa kupaki magari 1,000.

Kuhusu msaada waliopokea, aliwataka watumiaji wa vituo hivyo kuzingatia kunawa mikono, ili kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona na magonjwa mengine ya kuambukiza.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la WaterAids, Anna Mzinga, alisema msaada huo umegharimu Sh. milioni 106 na mashine hizo zimetengenezewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Naye Meneja Kituo cha Ubunifu na Uhawishaji Teknolojia cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Simon Marandu, alisema walitengeneza mashine hizo chini ya ufadhili wa Shirika la WaterAid..

# IMF yaisamehe Tanzania deni bil. 33/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS John Magufuli amelishukuru Shirika la Fedha Ulimwenguni (IMF), kuisamehe Tanzania deni la Dola za Marekani milioni 14.3 (sawa na Sh. bilioni 33.1).

Alitoa shukrani hizo jana wakati wa hafla ya uwekaji jiwe la msingi la ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mji wa Serikali, uzinduzi wa jengo la ofisi za Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (Tarura) na ugawaji wa pikipiki za maofisa tarafa.

Kadhalika, Rais Magufuli alisema anamuandikia barua Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo kumpongeza kwa kusamehe deni hilo.

"Leo hii hili Shirika limetangaza kuisamehe Tanzania deni lenye thamani ya Sh. bilioni 33.1 sawa na Dola za Kimarekani milioni 14.3 ambalo lilipaswa kulipwa ndani ya miezi minne ijayo, kuanzia Juni 10, 2020 hadi Oktoba 13, 2020," alisema.

Alibainisha kuwa IMF imechukua hatua hiyo kupitia Mfuko wake wa Catasrophe Containment and Relief Trust (CCRT) ili kuiwezesha Tanzania kukabiliana na athari za corona katika nyanja za kijamii na kiuchumi.

Alifafanua kuwa fedha hizo pamoja na mambo mengine zitatumika kupambana na corona na watashughulika na maeneo mengine ya miradi ya maendeleo ili corona ipotee kabisa.

Alisisitiza kuwa corona imepungua kwa kiwango kikubwa huku akiagiza Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kukiongezea bajeti kitengo cha dawa za asili.

Aliwasihi Watanzania kutodharau matumizi ya dawa za asili kipindi hichi cha corona.

"Endeleeni kuniombea na mimi nawaombea tunamshukuru Mungu mambo yanaendelea vizuri tusidharau dawa za kienyeji, uchawi tu ndio mbaya, ndiyo maana nimetoa maelekezo kitengo cha dawa asili kiendelezwe na bajeti iongezwe," alisema.

Kuhusu baadhi ya tabia watu wanaosema dawa hizo zimepitwa na wakati, alisema wao ndiyo wamepitwa na wakati.

"Tulipumbazwa sana tupende vyao badala ya vyetu, tupende dawa zetu vitengo vya dawa za asili na wanaofanya kazi halali za dawa asili wasapotiwe ndio maana hata nchi nyingine kuna madawa ya kienyeji kule," alisema.

**AONYA MAOFISA TARAFA**

Akizungumzia ugawaji pikipiki, Rais Magufuli aliwataka maofisa tarafa kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa na zisitumike kama daladala.

"Msitumie mkiwa mmelewa, kubeba mishikaki zitumike kwenye maendeleo, niwaombe wasimamizi kila ofisa tarafa akabidhiwe kwa maandishi ili ikipotea alipe maana hakuna vya bure Tanzania, hizi ni fedha za walipakodi nchini,"alisema.

Akizindua jengo la Tarura, Rais Magufuli alipongeza ujenzi huo huku akiwaonya kutotumia fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara kujenga majengo kwenye mikoa na wilaya.

Kadhalika, aliagiza Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) kukamilisha jengo lake kabla ya mwaka huu kwa kuwa tangu kuanzishwa kwake mwaka 2000 haina jengo.

Awali, Mtendaji Mkuu wa Tarura, Victor Seif, alisema katika mji wa serikali zinajengwa barabara zenye urefu wa kilomita 51.2 zitakazogharimu Sh. bilioni 89.1 na kukamilika ndani ya miezi 18.

Kuhusu ujenzi wa jengo la Tarura, Seif alisema jengo hilo limejengwa kwa mfumo a force account kwa gharama ya Sh. bilioni 1.968.

Alisema kukamilika kwa ujenzi huo kunaipunguzia Tarura Sh. milioni 463.7 ambazo zilikuwa zikitumika kulipa pango.

## Wamfagilia mkurugenzi kuwapa vijana ruzuku

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WAKAZI wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, wamempongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Anderson Msumba, kwa kutenga Sh. milioni 50 kila mwaka wa fedha kama ruzuku ya kilimo kwa ajili ya vijana wanaolima zaidi ya hekari tano za mazao ya biashara.

Fedha hizo zinatokana na mapato ya ndani ya Halmashauri hiyo, zimekuwa zikitengwa kila mwaka wa fedha kwa ajili ya kununua pembejeo za kilimo kama mbolea za kupandia (NPK), mahindi, mbegu za alizeti na sumu ya kuua wadudu wanaoshambulia pamba na kuzigawa kwa wakulima.

Walisema kitendo cha Mkurugenzi kutenga fedha za kununua pembejeo na kuwagawia vijana wanaojishughulisha na kilimo chenye tija kinatakiwa kuingwa na Halmashauri nyingine nchini.

## Nyamagana watatuliwa changamoto ya barabara

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

WANANCHI wa Mtaa wa Nyamazobe, Kata ya Mkolani, wilayani Nyamagana, mkoani Mwanza, waliokuwa hawana sehemu ya kupita kutokana na mtaa wao kutokuwa na barabara, hatimae serikali imekamilisha ujenzi wa barabara ya kilometa 2.38.

Barabara hiyo ilikuwa changamoto ya muda mrefu kwa wakazi wa maeneo hayo.

Wakizungumza wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wilaya ya Nyamagana ya utekelezaji wa miradi ya barabara inayosimamiwa na Tarura Jiji la Mwanza waliishukuru serikali baada ya kuwajengea barabara hiyo ya Nyamazobe-Kasese-Nyahingi itakayo rahisisha usafiri wakati wakitaka kupata huduma mbalimbali.

Kwa upande wake Meneja Tarura Jiji la Mwanza, Mhandisi Mohamed Muanda, alisema mradi wa ujenzi huo sehemu kubwa uanzishwaji wake umetokana na juhudi za wananchi wa mtaa huo.

## Watafiti wawapa ushauri wakulima

**Na Frank Kaundula ,MOROGORO**

WATAFITI kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Ilonga, wamewataka wakulima wa mazao mbalimbali Kanda ya Mshariki kuwa na tahadhari juu ya mabadiliko ya tabianchi kwa kufuata ushauri wa kitaalamu. Ushauri huo ulitolewa jana na Mkurugenzi TARI Ilonga kituo cha Kilosa, Dk. Joel Meliyo, kwa kusema ili kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, wakulima wanatakiwa kufuata ushauri wa kitaalamu.

“Kilimo ndiyo uti wa mgongo wa taifa letu, lakini kutokana na changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi ,wakulima wanatakiwa kuzalisha mazao yao kwa kufutata ushauri wa kitaalmu ili kuongeza tija ya uzalishaji huyo,” alisema Meliyo.

Dk Meliyo alisema kituo hicho kimeunganisha nguvu ya pamoja ili kuhakikisha teknolojia ya mbegu zilizofanyiwa utafiti zinawafikia wakulima kwa wakati ili waweze kulima kilimo chenye tija kwao na kuwa taifa zima kwa ujumla.

# Madiwani waunda kamati kudai posho

**Na Happy Severine, SIMIYU**

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi, mkoani Simiyu, wameunda kamati maalumu ya kuchunguza madai ya fedha za posho za vikao vyao.

Madiwani hao wanadai Sh. milioni 137, ambazo hawajalipwa tangu waingie madarakani miaka mitano.

Akizungumza juzi wakati wa hitimisho la kikao cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi, Richard Kiberiti, alisema kamati hiyo ndogo itachunguza sababu za madiwani kutolipwa stahiki zao.

Kiberiti ambaye ni Diwani wa Kata ya Gasuma, alisema kamati hiyo itafanya kazi ya kulinganisha makusanyo ya mapato ya halmashauri ya kila mwezi.

“Kuunda kwa kamati hii siyo kwamba tunakwenda kukamata, hapana. Tunakwenda kuchunguza tu na tutaangalia uhalisia wa mapato yanayoingia,” alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, James John, amekiri kuwapo kwa madai ya madiwani hao.

“Hizo milioni 137 ni madai ya vikao vyao. Halmashauri hatuna fedha, ila watalipwa kama alivyoelekeza Mkuu wa Mkoa (Anthony Mtaka).

“Serikali imeshazungumza na wafanyabiashara tunaowadai. Wakitulipa tutawalipa haraka ili shughuli nyingine ziendelee,” alisisitiza John.

Katika hatua nyingine, alisema ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya hiyo itaondoa changamoto zilizokuwapo.

Naye Katibu Tawala Msaidizi wa Serikali za Mitaa Mkoa wa Simiyu, Maganga Simon, akizungumzia madeni ya posho za madiwani, alisema: “Imeshaelekezwa na Mkuu wa Mkoa wetu wa Simiyu, haya madeni ya waheshimiwa madiwani lazima yalipwe.”

“Tena yatalipwa haraka,” Simon alifafanua wakati akitoa ujumbe wa serikali kwenye kikao cha mwisho cha madiwani, kilichofanyika Mjini Dutwa wilayani hapa.

Diwani wa Kata ya Sakwe, Subi Bunzari, alizungumzia maendeleo yaliyofikiwa katani mwake tangu aingie madarakani yakiwamo ya nishati ya umeme, huduma za kiafya kuboreshwa tofauti ikivyokuwa awali.

Kwa mujibu wa Diwani Bunzari, miundombinu ya barabara imeboreshwa, huku huduma ya maji kutoka Ziwa Victoria ikitazamiwa kuwafikia muda wowote.

“Nampongeza sana Rais Magufuli kwa uchapakazi wake. Ni jembe,” alisema diwani huyo wa Kata ya Sakwe, huku akiwashukuru wananchi kwa ushirikiano wao usiotiliwa shaka.



Diwani wa Kata ya Kigamboni jijini Dar es Salaam (CCM), Dotto Msawa, akizungumza na wananchi wa eneo lake, wakati akiwaaga na kuwashukuru baada ya kumaliza muda wake wa uongozi, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Washikiliwa madai kusafirisha bangi

**Na Julieth Mkireri, PWANI**

JESHI la Polisi mkoani Pwani linawashikilia watu watano pamoja na magari manne wakituhumiwa kusafirisha dawa za kulevya aina ya bangi zaidi ya magunia kumi.

Kamanda wa polisi mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema June 7, majira ya usiku maeneo ya Kibaha walimkamata Said Mohamed (43) mkazi wa Kipunguni B, jijini Dar es Salam akisafirisha bangi gunia kumi kwa kutumia gari lenye namba za usajili T852 AYV aina ya Toyota akitokea Mikumi kuelekea Dar es Salaam.

Aliwataja waliokamatwa ni Jeremia Samwel (29) na Faizia Kindamba (26) wakazi wa Mbagala jijini Dar es Salaam wa waliokamatwa eno la Ubena Chalinze wakisafirisha bangi iliyokadiriwa kuwa kilogramu 55 zikiwa zimefungwa kwenye mabegi makubwa manne na dogo moja wakiwa kwenye gari yenye namba za usajili T 809 DKQ aina ya Noah.

Alisema mtuhumiwa Alex Mkiri (43) alikamatiwa eneo la Bwawani Chalinze akisafirisha bhangi viroba vitano kwenye gari namba T 332 DLE aina ya Toyota IST kutoka Morogoro kwenda Dar es Salaam, na huko Picha ya Ndege Wilaya ya Kibaha.

Alisema ilikamatwa bajaji yenye namba za usajili TMC 484 AJJ, ikiwa na viroba viwili vikiwa na bhangi kilo 26, mtuhumiwa alitoroka kabla ya kukamatwa.

# Mbunge ashtushwa mrundikano wafungwa Gereza la Segerea

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Mariam Kisangi, amesema Gereza la Segerea lina mrundikano mkubwa wa wafungwa hali inayoweza kusababisha magonjwa ya mlipuko.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo la mrundikano wa wafungwa katika gereza hilo.

Katika majibu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ilisema Gereza la Mahabusu Segerea lilianzishwa mwaka 1995, huku likiwa na uwezo wa kuchukua kisheria jumla ya wahalifu 1,800.

"Kimsingi Gereza hilo lilianzishwa kwa lengo la kuwahifadhi mahabusu wenye kesi zao katika Mahakama mbalimbali," ilisema.

Hata hivyo ilisema kutokana na kasi ya ukuaji wa uchumi katika Mkoa wa Dar es Salaam, hali hiyo imesababisha ongezeko la uhalifu na kupelekea Gereza la Mahabusu Segerea kukabiliwa na changamoto ya msongamano wa mahabusu.

Kufuatia tatizo hilo, ilisema serikali kupitia Jeshi la Magereza imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kutatua tatizo hilo.

"Mathalani, kuwahamisha baadhi ya mahabusu kwenye magereza yenye nafasi, kuendelea kufanya mawasiliano na taasisi mbalimbali za kiuchunguzi na kimaamuzi zenye kuhusika na uendeshaji wa kesi za mahabusu ili mashauri yao yaweze kupatiwa ufumbuzi na kumalizika kwa wakati," ilisema.

Aidha, ilisema serikali ina mpango wa muda mrefu ambao ni kujenga magereza kila wilaya zisizokuwa na magereza kwa awamu ikiwemo Mkoa wa Dar es Salaam kadri ya hali ya bajeti itakavyoruhusu.



# Vipaumbele 6 kupunguza utapiamlo

**Na Augusta Njoji, DODOMA**



SERIKALI imetaja vipaumbele sita vinavyolenga kupunguza utapiamlo nchini ifikapo mwaka 2021.

Hayo yalibainishwa bungeni jana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Esther Mahawe.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema Mkoa wa Manyara una tatizo kubwa la utapiamlo kwa asilimia 36 jambo ambalo linasababisha udumavu hasa kwa watoto chini ya miaka mitano.

"Je, ni nini juhudi za serikali katika kuhakikisha tatizo hili linadhibitiwa?" alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema serikali imechukua juhudi mbalimbali katika kunusuru tatizo hilo ikiwa ni pamoja na kuandaa na kutekeleza Mpango Mkakati Jumuishi wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Afua za Lishe (National Multisectoral Nutrition Action Plan - NMNAP 2016/17-2021/22).

Ilisema mpango huo una vipaumbele vinavyolenga kupunguza utapiamlo ifikapo mwaka 2021.

Ilitaja vipaumbele hivyo kuwa ni kupunguza viwango vya udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kutoka asilimia 34 ya mwaka 2015 hadi asilimia 28.

"Kudhibiti viwango vya ukondefu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na kufanya viendelee kubakia chini ya asilimia 5 iliyopo sasa," ilisema.

Kingine ni kupunguza viwango vya watoto wanaozaliwa na uzito pungufu kutoka asilimia 7 ya mwaka 2015 hadi kifikia chini ya asilimia 5 na kupunguza idadi ya wanawake walio katika umri wa uzazi (miaka 15-49) wenye upungufu wa damu kutoka asilimia 44.7 ya mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 33.

"Kupunguza tatizo la upungufu wa Vitamini A kwa watoto wenye umri miezi 6 hadi 59 kutoka asilimia 33 ya mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 26, Kudhibiti tatizo la uzito uliozidi kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na kubakia kuwa chini ya asilimia tano," ilisema.

Hata hivyo, ilisema serikali ilianzisha muundo wa kada ya maofisa Lishe Wizara ya Afya mwaka 2012, ambapo jumla ya maofisa Lishe 114 wameajiriwa katika Mikoa na Halmashauri na Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais (Tamisemi).

"Taratibu zinaendelea kuwaombea vibali vya ajira wawe wengi zaidi. Aidha, serikali kwa kushirikiana na wadau wa Lishe imeazimia na inaendelea kutekeleza afua za lishe zenye matokeo makubwa," ilisema.

Ilitaja afua hizo kuwa ni pamoja na utoaji wa vidonge vya madini chuma na Asidi ya foliki kwa wajawazito, utoaji wa matone ya vitamin 'A' na dawa za minyoo.

Pia, uongezaji wa virutubishi vya madini na vitamin kwenye chakula hususan unga wa ngano, mahindi, mafuta ya kula pamoja na urutubishaji wa kibiologia wa mazao kama viazi vitamu, mahindi, maharage na mihogo, kutoa matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto wa chini ya miaka mitano.

"Nyingine ni utoaji elimu na huduma za lishe kwa wanawake, wasichana, watoto wachanga na wadogo, elimu ya ulaji vyakula mchanganyiko na mtindo bora wa maisha," ilisema.

# Bil. 85/- kodi ya majengo zakusanywa miaka mitatu

BUNGE limeelezwa kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu, kiasi cha Sh. bilioni 85.72 kimekusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kupitia kodi ya majengo.



Kiasi hicho kimekusanywa kwa 2016/17, 2017/18 na 2018/19, ikilinganishwa na Sh. bilioni 64.65 kilichokusanywa kupitia halmashauri zote nchini kwa kipindi cha miaka mitatu (2013/14, 2014/15 na 2015/16).

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Wizara ya Fedha na Mipango ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Suzana Mgonukulima.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema kuanzia mwaka 2015-2016 Bunge lilipitisha Sheria ya ukusanyaji wa Kodi ya Majengo kupitia TRA.

"Je, hadi sasa suala hili limeleta tija gani kwa Serikali?" alihoji.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilisema serikali ilianza kukusanya kodi ya majengo kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuanzia mwezi Oktoba, 2016 baada ya Bunge kupitisha Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016 ambapo Sheria ya Kodi ya Mamlaka ya Miji, Sura 289 ilifanyiwa marekebisho na kuhamishia jukumu hilo chini ya TRA.

"Kufuatia marekebisho hayo ambayo yaliipa TRA jukumu la kukusanya kodi ya majengo, makusanyo ya kodi hiyo kwa mwaka 2016/17 yaliongezeka hadi kufikia Sh. bilioni 34.09 kwa halmashauri 32 za Tanzania Bara ikilinganishwa na makusanyo ya Sh. bilioni 28.28 ya kodi hiyo kwa mwaka 2015/16 kwa Halmashauri hizo," ilisema.

Hata hivyo, ilisema marekebisho ya Sheria yaliyofanyika kuipa TRA jukumu la kukusanya kodi hiyo yameleta tija kubwa kwa serikali kutokana makusanyo yameongezeka ikilinganishwa na hapo awali ambapo kodi hiyo ilipokuwa ikikusanywa na halmashauri zenyewe.




Ukurasa 13

Mbona bila vyama vya siasa inawezekana! -2

BUFE
IJUMAA JUNI 12, 2020
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 12

## Mradi gesi kinyesi unavyohamisha wananchi kutoka umaskini wa kuni

MTAZAMO WA DUNIA

# Uchumi baada corona, dira kuzalisha zaidi, mahitaji...



Wajasiriamali wakiendelea na biashara ya nguo za mitumba, inayoajiri wengi katika sekta isiyo rasmi nchini. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Nimi Mweta**

MABADILIKO yameanza kuonekana katika ushirikiano wa uchumi na mbinu za kukuza uchumi, kila nchi baada ya mtikisiko wa ugonjwa corona, huku shughuli za uchumi katika nchi za Magharibi zikionekana bayana kuamka.

Yako maeneo yanayobadilika haraka 'makwetu' kupunguza viwango vya uliberali katika sera na kukazia uzalishaji wa ndani, kusimamia ubora wa viwango. Hali hiyo inajionyesha kwa majirani, mfano eneo la usafirishaji.

Hata katika kudhibiti kuenea ugonjwa huo, serikali nchini ilianza kuwa makini na uingizaji vifaa vya kutumia kujilinda na maambukizo, visiingizwe kiholela kutoka nje.

Uzalishaji wa ndani ukapungua. Ndani ya muda mfupi, ilionekana utengenezaji vifaa kama barakoa unawaokoa baadhi ya wajasiriamali ambao shughuli zao zimedoda.

Kupungua uingizaji fedha kutoka nje baada ya usafiri kupungua kwa sehemu kubwa na kuathiri sekta ya utaliii inayoingiza fedha nyingi nchini, hatua zimeanza kuchukuliwa kupunguza ushindani kati ya bidhaa za matumizi ya kila siku zinazotoka nje.

Mojawapo ni maziwa. Waziri wa Mifugo na Uvuvi Luhaga Mpina, hivi karibuni alitangaza operesheni msako wa mwezi mmoja kudhibiti uingizaji holela wa maziwa na mifugo kutoka nje, ili kulinda soko la ndani la maziwa.

Pia, kuna hatua ya kiwanda cha kusindika nyama zimeanza maeneo ya Kibaha kukidhi mahitaji ya soko nchini na kimataifa.

Taasisi za serikali zinahakikisha zinatumia maziwa kutoka wazalishaji wa ndani siyo nje, katika hatua inayoonyesha dhamira katika utendaji wa sera ya kulinda viwanda, inayopaswa kuwa ya dhati.

Mazingira ya Covid-19 yamepunguza kwa kiwango kikubwa kuwapo utandawazi katika biashara na mwingiliano wa namna nyingine, kubakiza tu uwezo wa mawasiliano katika mitandao.

Kupungua kwa mahitaji kumelazimisha kuangalia kodi zinazotozwa hapa na pale, kutoa nafasi kwa wazalishaji kumudu; benki kupunguza riba, kuongeza muda mikopo.

Marekani, nchi kigogo wa ukubwa wa uchumi duniani, imepoteza takriban robo ya ajira zilizokuwapo kuelekea mwisho wa mwaka jana, na licha ya kupanda kidogo kwa ajira mwezi Mei, bado hali imebaki kama ilivyo wakati milango inafunguliwa tena.

Viwanda kutumia maroboti (mashine za kupeleka au kupokea vitu kwa kutembea kama binadamu) kunatarajiwa kuongezeka na walio na umri mkubwa watapoteza kasi kwa kiasi kikubwa.

Tayari vyuo vikuu nchini Afrika Kusini, vikitafakari kuendelea na masomo, vilisema walio na miaka 65 au zaidi wasirudi kabisa katika vitivo, wabaki nyumbani. Watafundisha kutoka huko au ndiyo kustaafu?

Pia, kuna tatizo limaloibuka la kutoa ajira, kwani zinakuwa chache zaidi kuliko awali na kila nchi ina nyufa zake za mshikamano zinazoleta ubaguzi, hali inayoashiria kuvurugika zaidi kwa utawala barani Afrika.

Kupungua soko la nje kwa mazao kadhaa, ikiwemo pamba kunafanya serikali iweke mkazo katika utengenezaji wa bidhaa za pamba na hasa nguo, kuacha kuzinunua kutoka nje ili kuwe na soko la bidhaa za kilimo nchini.

Wakati pingamizi kubwa iliyopo ni kuvuruga ajira ya sekta isiyo rasmi ambayo kwa kiwango kikubwa inategemea mauzo ya bidhaa kama za nguo kutoka nje ambako zinalipiwa tu gharama za usafirishaji kutoka ng'ambo, inakuwa kitendawili cha kiuchumi kfanyiwa kazi.

Mwaka 2016 nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), zilifikia uamuzi kama huo, lakini baadaye kukavurugika jambo.

Rwanda ndiyo mwanachama pekee wa EAC aliyeendelea na sera ya kuondoa bidhaa 'mitumba' sokoni na kweli imeondolewa katika orodha ya washiriki wa AGOA (sera ya Marekani ya bidhaa za Afrika takriban 350 kuingia bila ushuru wa forodha).

Rwanda ni nchi ndogo na inawezekana soko la Umoja wa Ulaya la vigezo hivyo linaloitwa EBA (Eveything But Arms) linatosha kwa bidhaa zake.

UCHUMI

# Mradi gesi kinyesi unavyohamisha wananchi kutoka umaskini wa kuni

**Na Beatrice Shayo**

NARIRI MATHAYO (43), ni mwanamke mwenye watoto watano. Ili apate nishati ya kupikia nyumbani, inamlazimu aamke alfajiri kila siku kwenda kufuata kuni.

Anasimulia kwamba alikuwa anatumia saa tano kufuata kuni kila siku na kuna wakati alirudi nyumbani na mzigo 'kiduchu; kutokana na wingi wa wasaka kuni.

Nariri anayeishi kwenye nyumba ya udongo kijiji cha Oldonyowas katika Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, anasema ni safari iliyomchosha mno, katika maisha yake ya kila siku.

"Kuna muda mvua ikinyesha, huwezi kwenda msituni kutafuta kuni hii...inanibidi nikanunue kuni nne kwa Sh 1,000 ili niweze kupika na maisha ya hapa kijijini ni magumu, kuipata hiyo hela ni mtihani," anasema.

**MAISHA MAPYA**

Kama ulivyo usemi kila jambo lina mwisho, safari ndefu za Nariri kutafuta kuni, sasa zimeisha baada ya kuanza kutumia nishati ya kinyesi cha ng'ombe maarufu kama baiogesi.

"Nilivyoanza kutumia baiogesi kama nishati mbadala kwa ajili ya kupikia baada ya kuhamasishwa, nikaona ni mkombozi wa maisha yangu. Saa tano ni nyingi kupoteza kila siku," anaeleza.

Kijiji Oldonyowas, kilianzishwa mwaka 1975, zao la operesheni vijiji, umbali wa kilomita 35 kutoka mjini Arusha. Bado hakina umeme licha ya kuwepo nguzo kubwa inayopita kijijini hapo.

Arusha, imo katika orodha ya mikoa inayotumia kuni kwa asilimia 61.3 ya wakazi, nyuma ya Simiyu inayoshika nafasi ya kwanza kwa asilimia 94.3, kwa mujibu wa Ripoti ya Upatikanaji Nishati Tanzania Bara, 2016 ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Baada ya kubainika ukataji mkubwa wa miti kijijini hapo, ilitafutwa njia mbadala kuwasaidia wananchi, ambayo ni kinyesi cha ng'ombe.

Kampuni ya Oikos yenye makao makuu nchini Italia, ilifadhili mtambo wa baiogesi kwa gharama ya Sh. milioni 2.5 na wananchi walitakiwa kulipa kwa Sh 215,000. Lengo ni kutetea mazingira yao.

"Mwaka jana nimeanza kutumia nishati mbadala ya kinyesi cha ng'ombe nililipa Sh. 215,000 kwa ajili ya kupatiwa vifaa kama mabomba na jiko la kupika," anasema.

Mama huyo anaeleza muda aliyotumia kutafuta kuni, sasa anatumia kwa shughuli nyingine kama vile kilimo na kupika chakula kwa wakati.



Mwanamama akiwa katika mtambo unaompatia nishati ya gesi itokanayo na kinyesi cha mifugo. Picha ndogo, jiko la gesi inayotumia nishati ya kinyesi cha wanyama. **PICHA: BEARTICE SHAYO.**

> **"Wenye mradi walikuwa wakitafuta kampuni baada ya kutangaza, nilipatikana mimi na kazi kubwa niliyopewa ni kuwaelimisha wananchi kuhusiana na nishati mbadala, nikamjenga mmoja na wengine wakapenda," anasema Ombeni Urio, Msimamizi wa Ujenzi wa Mtambo wa Baiogesi.**

Ili mtambo huo ufanye kazi, Nariri anasema anatakiwa kuweka ndoo tatu za kinyesi laini cha ng'ombe.

"Huwa najitahidi kuhakikisha kila siku nalisha mtambo ili nipate gesi nyingi ukiweka kinyesi kidogo utapata gesi ndogo," anasema.

**ALIVYOJIUNGA**

Katika kuhakikisha anaipata nishati hiyo ya kupika, ilimbidi aende kukopa kiasi cha Sh 115,000 kwenye kikundi, kwani haikuwa rahisi kupata fedha hiyo kwa mkupuo.

"Niliuza mboga na mayai kupata marejesho haikuwa ni jambo rahisi naamini ilikuwa ni mipango ya Mungu kuipata hii baiogesi," anasema Nariri, akifafanua mkopo unaopaswa kurejeshwa katika miezui sita.

**MAGEUZI KIJIJINI**

Matumizi ya baiogesi yamefanya wanakijiji hao kupunguza gharama za maisha, wanaokoa fedha za kuinunua kuni na wanazitumia kwa mengine ya maendeleo.

Neema Lucas, ni mwanakijiji anayesema walikuwa wananunua kuni za Sh.12, 000 kwa wiki hivyo tangu wamepata biogesi hawanunui tena wala kwenda kutafuta kuni.



Mwanakijiji akitoka kukata kuni, kabla kuanza kutumia gesi itokanayo na nishati ya kinyesi cha wanyama.

Licha ya kuwa ni mwanamke wa kawaida, Neema ana ujuzi kafunzwa taaluma kwa mapana, ikiwamo kujua kiwango cha gesi.

"Ili ujue gesi ipo nyingi itaanza kusoma kuanzia namba nne na kuendelea na pale unapokuwa mdogo inakulazimu kuweka kinyesi," anasema kwa kujiamini huku akitaja changomoto inayowakabili sasa ni ulegevu wa mabomba unaosababisha upotevu wa gesi.

Wanufaika wakuu wa mradi ni wenye mifugo mingi inayozalisha kwa wingi kinyesi kupata nishati hiyo.

Donatha Abraham, anasema kutokana na wingi wa ng'ombe zake, imekuwa rahisi kupata kinyesi kwa wakati kulisha mtambo.

"Ni bora kujaza kinyesi katika mtambo kuliko ule umbali wa kutafuta kuni si unajua hawa wanaume zetu haijalishi ni mjamzito utakwenda kutafuta kuni... nilikuwa nachoka ukiwa na ujauzito uende huko msituni acha tu ...hii nishati imenisaidia," anasema.

Kwa sasa mama huyo anasema anapata angalau muda wa kufanya shughuli zake nyingine.

**GHARAMA KIKAWZO**

Wakati wengine wapo wanaopambana hadi kukopa ili kupata baiogas, Monica Mollel kwake yote yameshindikana na kumfanya aendele kuiona kwa jirani, binafsi anabaki kwenye kuni.

Mollel anasema kipato chake ni kidogo na kuna wakati anakosa kutimiza milo ya chakula hivyo hatoweza kumudu biogas.

"Nashindwa kuweka akiba ya kulipia hizo gharama ila napenda kutumia hiyo nishati maana naona wenzangu inawasaidia hawaendi tena kukata kuni," anasema Magdalena Loshije.

Magdalena anasema, wao kinamama wa jamii ya kimasai wanategemea vibarua vya kilimo cha karoti na fedha anayoipata inaishia kulisha watoto, kugharamia masomo na mahitaji madogo.

**MASAHIBU YA KUNI**

Kwa wanaoendelea na ukataji kuni kutokana na kukosa nishati ya baiogasi, wanalalamika kukutana na masahibu lukuki mengine yakihatarisha maisha yao.

Paulina Julias, anasimulia aliambiwa 'aruke vichura' akamjulisha kuwa hawezi ni bora akachapwa wakamsamehe.

"Wakati mwingine ukishindwa hizo adhabu inamuweka mtu katika mazingira ya kubakwa, mbali na hilo tunaumia wakati unakata kuni huko msituni na wakati mwingine tunarudi na vidonda," anasema.

**WAWEKEZAJI JE?**

Ili kutekeleza mradi huo Oikos, ilitafuta kampuni ya ujenzi ambayo iliyotoa mafunzo kuhamasisha wananchi kutumia nishati hiyo na kuwajengia mtambo wa baiogesi.

"Wenye mradi walikuwa wakitafuta kampuni baada ya kutangaza, nilipatikana mimi na kazi kubwa niliyopewa ni kuwaelimisha wananchi kuhusiana na nishati mbadala, nikamjenga mmoja na wengine wakapenda," anasema Ombeni Urio, Msimamizi wa Ujenzi wa Mtambo wa Baiogesi.

Urio anasema mradi ulikuwa wa bure kwa wananchi, waliotakiwa kuwa na mawe pamoja na kuchimba shimo.

Anasema baadhi ya wananchi waliona usumbufu kuzoa kinyesi na kukikoroga, kwamba kazi ngumu, kwani ni lazima uwekewe kinyesi ili kiweze kuzalisha na mtu anapona usumbufu, uhai wa mtambo unaigia hatarini.

**VIONGOZI KIJIJI**

Pamoja na kuwapo mitambo hiyo, viongozi wa kijiji hicho wanasema hawajui ni wangapi waliofungiwa nishati hiyo.

Mwenyekiti wa kijij, Laran Mollel, anasema hana takwimu halisi ya wananchi waliofungiwa mtambo huo wa nishati mbadala kijiji kwake, kunakokadiriwa kuwa na jumla ya wakazi zaidi ya 4,000.

Anasema, Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, inaonyesha kijiji kilikuwa na watu 2,544 wanawake 1,331 na wanaume 1,213.

"Sehemu kubwa ya hiki kijiji hakina umeme licha ya nyaya kupita hapa...wengi wao tumeambiwa tutaletewa umeme mpaka sasa bado," anasema Ofisa Mtendaji wa Oldonyowas, Jenifer Mcharo.

**WATAALAMU**

Ofisa Mradi wa Nishati Safi na Usawa (TANGSEN), Thabit Mikidadi, anasema gharama walizopewa ni nafuu kwa mitambo ya baiogesi inauzwa gharama kubwa kuanzia Sh.700, 000.

"Kama wamefadhiliwa sio jambo baya wafadhili wengi wanataka ulipie hata kidogo, ili uwe na uchungu nacho katika kukitunza bila hivyo hao wananchi hawataithamini hiyo baiogesi," anasema.

Mikidadi anasema kuna mambo mawili kuendeleza baiogesi, la kwanza ni kutoa elimu kwa wenye kipato katika familia kuhusu umuhimu wa nishati hiyo ambayo ni rahisi katika matumizi.

Anaendelea: "Njia nyingine wanaweza kusaidiwa kulipa kidogo kidogo kwa muda utakaopangwa kuliko kulipa fedha zote kwa wakati mmoja."

**DC MURO**

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, anasema matarajio ni kuleza wafadhili ili wasaidie kijiji hicho ili kinyesi cha ng'ombe kiwe mbadala wa ukataji wa kuni.

Anasema mradi ulipokwisha wananchi wameibuka na changamoto ya uelewa jinsi ya mradi kuwa endelevu na wengine wamebaki kuitegemea serikali na wadau wa maendeleo kutaka wasaidiwe muda wote.

Muro anasema, mradi umelenga kufikia kaya 15,000 kwa awamu kutegemea na fedha ya mfadhili na kwa sasa umetekelezwa kwa asilimia 85 na utakuwa ni endelevu.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Mbona bila vyama vya siasa inawezekana! -2






NA JOSEPH KULANGWA

WIKI iliyopita tuliona Tume ya Kutafuta Maoni ya kuwa na mfumo wa vyama vingi vya siasa ikiundwa. Nini kilifuata? Endelea...

Tume hiyo chini ya Jaji Mkuu Mstaafu Francis Nyalali, ikazunguka nchi nzima kuuliza Watanzania. Ikaja na jibu, kwamba hawataki.

Wanataka chama kimoja tu.Yaani wanaitaka CCM iendelee kuwa tawala. Asilimia 20 tu ndio waliokuwa wanataka vyama vingi.

Wenye akili zao wakakaa na kuona busara inalalia wapi, akiwamo Mwalimu Julius Nyerere. Wakashawishiwa na asilimia 20, wengi wape, lakini wachache wasikilizwe.

Wachache wakasikilizwa kwa mujibu wa muktadha wa wakati ule. Tukarejea rasmi kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992.

Waliokuwa na uzoefu wa vyama vingi huko nyuma, wakarejea ulingoni na kushirikisha wapya na haraka wakaunda vyama vyao baada ya muswada kupitishwa bungeni. Uchaguzi mkuu wa kwanza kuhusisha vyama vingi vya siasa ukafanyika mwaka 1995.

Wanasiasa Augustino Mrema na Profesa Ibrahim Lipumba, ni baadhi ya wapinzani walioshiriki uchaguzi huo uliomshuhudia Benjamin Mkapa wa CCM akiibuka mshindi.

Uchaguzi mwingine ukafanyika mwaka 2000, Mkapa tena akashinda kuwa Rais. Mwingine 2005, JakayaKikwete wa CCM akashinda, akafanya hivyo tena mwaka 2010.

Uchaguzi wa mwaka 2015 ukamshuhudia Dk. John Magufuli wa CCM tena, akiibuka kidedea. Bila shaka mwaka huu atasimama tena.

Tusubiri kuona nini kitajiri kwa ajili ya miaka mingine mitano ijayo. Akishinda itakuwa ya mwisho kwake na kupisha wengine.

Kwa kuwa siko darasani kudadavua kila kitu cha historia ya nchi hii, itoshe tu kwa ufupi wa tulikotoka Watanzania. Hivi sasa tuna vyama vya siasa 19 vikiendelea kutawaliwa na CCM.

Yaani vyama vya upinzani 18 na vyote vinapigana kuiondoa CCM madarakani. Katika hivyo, vipo vikubwa na vipo vidogo. Vipo makini na vipo bora liende, bora tupo. Vipo vyenye wabunge na vipo vyenye mbunge na vipo visivyo na mbunge.

Lakini vyote ni vyama halali vya siasa na vinashiriki siasa za nchi hii, vina wanachama, wafuasi, mashabiki na viongozi.

Vipo vinavyopata ruzuku kwa mujibu wa idadi ya wabunge, vipo visivyopata ruzuku kwa kukosa wabunge, yaani vina vyanzo vyao vya mapato, pengine ni ada za uanachama, michango au ufadhili, lakini vipo na hujibainisha zaidi nyakati za uchaguzi.

Licha ya udogo wa baadhi ya vyama, lakini hudiriki kusimamisha wagombea udiwani, ubunge na urais nyakati za uchaguzi mkuu, pamoja na wa serikali za mitaa, kwa sababu vina haki na uhalali wa kufanya hivyo.

Enzi hizo, TANU na ASP vilijijengea umaarufu ngazi zote, kuanzia mitaani, vijijini hadi Taifa. Ni wapi Bara mtu alikwenda na kutamka TANU watu wasiijue, ikiimbwa na kila mtu "Eee TANU yajenga nchi..." ASP vivyo hivyo kwa Zanzibar.

Katika vyama vya siasa 19 vilivyopo nchini leo, vipo baadhi ukienda vijijini na kuvitamka, unaweza usimpate mtu anayevijua, kwa sababu havipo, vinaishia mijini.

Si kwa kupenda, bali ni kutokana na ukata, haviwezi kujitangaza, haviwezi kuwafikia wanancni hata kwa kupitia vyombo vya habari. Havina nguvu.

Vyenye nguvu kila kukicha ni mapambano, hiki hakitaki kile kisa alie madarakani na kile hakitaki hiki kingie madarakani.

Hiki hakitaki kikosolewe, kile hakitaki kikemewe. Ili mradi kila kukicha ni ugomvi na kelele, huku maendeleo ya wananchi yakikwazika.

Tunashuhudia, vyama vingine vinakwazwa katika kujitangaza kwa njia za mikutano ya hadhara, kwa kinachoelezwa ni kupisha kingine kutekeleza Ilani ya uchaguzi! Kinachokatazwa kufanya siasa, kinalalamika kwamba kitakiondoaje chama kingine kisipofuata wananchi ambao ni wanachama wake?

Kinalalamika, kitajijengaje kama hakitashawishi wanachama wapya? Matokeo yake kinabaki kinagwaya na kujisalimisha jumuiya ya kimataifa kuishitakia serikali na kuomba nchi isipewe misaada.

Adui mwombee njaa umshinde na umwangushe na ndilo lengo. Hiyo ina maana ni athari mbaya kwa nchi, ina athari hasi kwa ustawi wa watu, bila kujali itikadi.

Inafikirisha, je, ni nini faida ya mfumo wa vyama vingi vya siasa. Je kuna faida ya kuwa na vyama vya siasa? Kwanini tunachaguana kwa misingi ya vyama?

Linakuja hitimisho linalohoji, je, kwani tukichaguana kwa uwezo bila vyama kuna tatizo? Hatuoni kuwa uwepo wa vyama vya siasa nchini kwa sasa unatuchelewesha maendeleo? Kwani Dk. Magufuli asingekuwa wa CCM au chama chochote tukamchagua urais asingefanya anayoyafanya?

Hebu sasa tujaribu kuchaguana kwa kuangalia uwezo wa mgombea, kwa sababu tunafahamiana.

Tufute vyama vya siasa tubaki na Tanzania. Si lazima tuige kwa jirani namna ya kuishi. Ni tafakuri tu, msiniangalie kwa macho mekundu mkanishughulikia kijadi. Alamsiki!

**• Simu: (+255) 0713 410008 jkulangwa@yahoo.com**

UCHUMI

# Kilolo yajipanga kuitumia Hifadhi Udzungwa iwatoe kiuchumi mkoa

- Yanuia kuwa wilaya ya kitalii, hoteli kibao
- Eneo 80%, kimapato haijaifikia Kilombero




NA FRANCIS GODWIN, IRINGA

MILIMA ya Udzungwa ni jina la Hifadhi ta Taifa iliyoko wilayani Kilolo, mkoani Iringa. Mtazamo uliopo mahali hapo, ni iwapo utawekewa mikakati ya vutia watalii, itaongeza uchumi wa wilaya na kuondoa umaskini wa mtu mmoja mmoja.

Pia, kwa upande mwingine, wilaya ya Kilombero mkoa wa Morogoro, nayo inamiliki sehemu ya Hifadhi ya Udzungwa kwa kitumia vyema eneo dogo ililo nalo, kuliganisha, lakini inajulikana zaidiipande wa Morogoro.

Jitihada za serikali ya wilaya ya Kilolo, chini ya Mkuu wa Wilaya, Asia Abdalah na Kamati ya Utalii, inanuia kuona hifadhi za mkoa wa Iringa, ikiwamo Udzungwa, zinajulikana.

Hifadhi hiyo iko umbali wa kilometa 350 Kusini mwa jiji la Dar es Salaam na kilometa 65 kutoka Hifadhi ya Taifa ya Mikumi,

Jina la hifadhi limetokana na milima hiyo ya Udzungwa, yaani nchi ya Wadzungwa, tawi la Wahehe. Ina ukubwa wa kilometa mraba 1990, ikiwa na hazina nyingi za mimea, ndege na wanyama wasiopatikana kokote kwingine duniani.

Wahifadhi wanafafanua kuna aina 11 za jamii ya nyani wa kipekee, wawili wanapatikana Udzungwa pekee, akiwataja ni Mbega Mwekundu wa Iringa, aliyekuwa hajulikani mpaka mwaka 1979.

Kuna aina nyingine nne za ndege ambao ni: Chozi Bawa Jekundu (rufous-winged sunbrid) na jamii mpya iliyogunduliwa ya aina ya Kwale wa Udzungwa, zinazofanya hifadhi kuwa makazi rasmi na muhimu kwa ndege pori barani Afrika.

> **"Ndoto yangu kuona asilimia 80 za hifadhi hii zilizopo Kilolo zinakuza uchumi wa wana Kilolo na Taifa kwa ujumla. Nimetembea zaidi ya saa sita kupanda na kushuka mlima Udzungwa upande wa Kilombero mkoa wa Morogoro."**

Pia, kuna wanyama kama simba, chui, nyati na tembo. Huku kukiwepo mimea inayopatikana katikati ya miti mirefu inayofikia mita 30.

Mkuu wa Wilaya anautaja, Mto Sanje, ni kivutio kikubwa chenye maporomoko ya maji yenye urefu wa mita zipatazo 170, kupitia msituni.

**UTAJIRI WAKE**

Mkuu wa Wilaya, Asia Abdallah, anasema manufaa ya Udzungwa yataonekana iwapo Kilolo na mkoa wa Iringa utajipanga katika miundombinu,kuvutia wawekezaji kujenga hoteli za kitalii za kuvutia watali kutembelea Udzungwa, upande wa Kilolo, Iringa.

"Ndoto yangu kuona asilimia 80 za hifadhi hii zilizopo Kilolo zinakuza uchumi wa wana Kilolo na Taifa kwa ujumla. Nimetembea zaidi ya saa sita kupanda na kushuka mlima Udzungwa upande wa Kilombero mkoa wa Morogoro.

"Hifadhi ya Taifa ya Udzungwa, kuwa kuna maeneo mazuri ya wawekezaji kujenga hoteli ila hadi sasa bado changamoto ya hoteli inakwamisha watalii kufika Kilolo," anasema.

Asia anasema engo ya ziara yake hiyo ni kujifunza na kuona ni kwa kiasi gani hifadhi ya Udzungwa itanufaisha wananchi wa Kilolo kwa kupata wawekezaji zaidi.

Inaelezwa, kuwepo hoteli nyingi upande wa Kilombero kumetoa fursa kwa wananchi wake kunufaika zaidi, jambo ambalo sasa linapaswa kuhamishiwa Iringa na mahsusi Kilolo.

Anasema, serikali mkoa wa Iringa imeweka mkakati wa kufungua lango la utalii mikoa ya Kusini na tayari imefunguliwa mwaka jana.

Aliyekuwa kuu wa Mkoa wa Iringa, Amina Masenza, anasema kuwa eneo la ujenzi wa kituo cha utalii kwa mikoa ya Kusini (southern circuit) kumetengwa eneo la kihisa Iringa na itapewa jina la 'Karibu Kusini.'

**WENYE HIFADHI**

Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Udzungwa, Hassan Nguluma, anasema upo mkakati wa kuboresha miundombinu upande wa Kilolo, kuvutia wawekezaji.

Anasema, asilimia 20 ya hifadhi hiyo ipo wilayani Kilombero na asilimia 80 zilizobaki ziko wilaya ya Kilolo, ambako kuna wanyama wa kila aina huku upande wa Kilombero, zaidi ni vivutio vya maporomoko mazuri ya maji.

Kuhusu idadi ya watalii, anasema wapo kutoka ndani ya nchi hasa wanafunzi na wageni kutoka nje, japo changamoto kubwa huwa katika kipindi cha masika, miundombinu hasa ya barabara inakuwa katika hali mbaya, japo anakiri serikali iko mbioni kuanza ujenzi wa barabara ya lami.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Dk. Allan Kijazi, anasema kuwa mkakati wa kuvutia utalii katika mikoa ya Kusini, umeanza ili watalii wengi wapendelee kufika hifadhi za Kusini mwa nchi.

Anasema gharama kubwa ya nauli ya ndege kutoka Dar es Salaam hadi mkoani Iringa, ni sawa na nauli ya kutoka Dar es Salaam kwenda Dubai, inawafanya watalii kutopenda kufika mikoa ya Kusini.

Rai yake ni kuboreshwa Uwanja wa Ndege wa Nduli, mjini Iringa, utakuwa na maana kubwa kuongeza idadi ya watalii katika hifadhi hizo za Kusini .

**Mwandishi anapatikana kwa simu 0754026299 barua pepe ; francisgodwin2004@yahoo.com**



Mandhari ya Hifadhi ya Taifa ya Udzungwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**





# Hati safi Jiji Dodoma yamkuna Mahenge

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameridhishwa na utendaji kazi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kutokana na kupata hati safi katika ukaguzi wa hesabu za serikali za mwaka 2018/2019.

Kauli hiyo aliitoa katika mkutano wa Baraza la Madiwani kupitia taarifa ya Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa hesabu za Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2019.

Dk. Mahenge alisema Halmashauri ya Jiji la Dodoma imepata hati safi kwa ukaguzi wa hesabu za mwaka 2018/2019.

"Niwapongeze kwa dhati kwa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa kazi nzuri mliyoifanya kwa kipindi chenu cha miaka mitano mpaka Jiji la Dodoma linapendeza, hongereni sana," alisema Dk. Mahenge.

Alisema hakuna kilichotekelezwa bila kupitia vikao vya Baraza la Madiwani, baraza hilo ni sehemu ya mafanikio yote yaliyofanyika hapa Dodoma.

Akizungumzia hoja 46 za ukaguzi zilizopatikana, Mkuu wa Mkoa aliwataka kuzitatua hoja hizo.

"Ukiziangalia hoja hizi za CAG, zaidi ya asilimia 80 ninyi wenyewe mnaweza kuzitatua ni asilimia ndogo tu ambayo ndiyo inahitaji ngazi ya juu kama upungufu wa watumishi kwenye sekta ya afya," alisema Dk. Mahenge.

Alisema wanatakiwa kuweka mkakati na ratiba ya kuhakikisha hoja zote zinajibiwa, hoja zilizo nje ya uwezo wa Jiji, Serikali ya Mkoa itaendelea kushirikiana katika kuzitatua.

Akiwasilisha taarifa ya CAG kwa hesabu za Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2019, Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, alisema Halmashauri ya Jiji la Dodoma ina jumla ya hoja 46 kwa mwaka 2018/2019.

Katika hoja hizo, 12 ni za miaka ya nyuma na 34 ni hoja za mwaka 2018/2019.

"Mheshimiwa mwenyekiti, tumeweza kupunguza hoja za ukaguzi kwa kiwango cha hoja 11 ukilinganisha na mwaka 2017/2018 ambapo tulikuwa na jumla ya hoja 57. Mheshimiwa mwenyekiti, hoja zote zimejibiwa na kuwasilishwa kwa mkaguzi wa nje ndani ya siku 21 kama inavyotakiwa kwa mujibu wa sheria," alisema Kunambi.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa katika ukaguzi wa hesabu za mwaka 2018/2019, CAG ametoa hati safi.

Alisema hati hii inalifanya Jiji la Dodoma kuendelea kupata hati safi toka mwaka 2016/2017 hadi 2018/2019.

"Nichukue nafasi hii kuipongeza kwa dhati timu yangu mahiri ya wakuu wa idara na vitengo wa Jiji la Dodoma kweli wamefanya kazi nzuri maana msingi wa hoja unatoka kwenye idara na mimi kama ofisa masuuli, ninafanya matumizi ya idara zote, kama mkuu wa idara asipokuwa makini kunishauri kwenye eneo lake tunatengeneza hoja nyingi zaidi," alisema Kunambi.

# Bahi wamwomba JPM kutatua mgogoro ardhi

**Na Paul Mabeja, BAHI**

WAKAZI wa Kijiji cha Nghulugano, wilayani Bahi mkoani Dodoma wamemwomba Rais John Magufuli, kuingilia kati mgogoro wa ardhi ulipo kati yao na serikali ya kijiji kutokana na walimu wa shule ya msingi kupora zaidi ya hekari 50, za mashamba yao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika kijiji hicho, juzi, wakazi hao walidai uongozi wa kijiji kwa kushirikiana na ule wa Shule ya Msingi Nghulugano, wamepora maeneo yao waliyokuwa wakiyategemea kwa ajili ya kilimo.

Mmoja wa wakazi hao, Therezia Manala, alisema maeneo yao yamechukuliwa na walimu wa shule hiyo bila wao kushirikishwa na kila wanapodai kurudishiwa wanaelezwa kuwa hilo ni eneo la taasisi.

Manala, alisema kuwa maeneo hayo ambayo wamekuwa wakiyamiliki kwa muda mrefu wanashangaa kuona kuwa uongozi wa shule umeyahodhi bila kufuata utaratibu wowote.

"Tunaambiwa haya maeneo ambayo tulikuwa tunayalima kuwa ni eneo la taasisi, lakini humo yapo hadi makaburi ya ndugu zetu ambao tumewazika lakini wameyapuuza na kuyalima kwa trekta bila kujali," alisema.

Naye Bosco Amandus, alisema walimu wa shule hiyo wamechukua maeneo yao ambayo walikuwa wanayalima na kugawana kwa ajili ya kufanya shughuli za kilimo wao binafsi.

Amandusi, alisema wanamwomba Rais Magufuli, kuingilia kati mgogoro huo kwa kuwa walimu wamepora maeneo yao kwa madai kuwa ni ya taasisi.

"Shule hii imekuwa kama Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), walimu wamechukua maeneo yetu ya mashamba na kujimilikisha kwa ajili ya kulima wao binafsi wamelima hadi makaburi yetu yaliyokuwapo awali na kama kweli hili wanasema ni eneo la taasisi ilikuaje sisi kuzika ndugu zetu humo, tunaomba serikali iliangalie hili," alisema Amandusi.

John Chitinde, alisema malalamiko yao yamekuwa ya muda mrefu, lakini viongozi wa kijiji pamoja na wa ngazi ya juu wamekuwa wakiwapiga danadana kuwatatulia kero hiyo hali ambayo inawalazimu sasa kutaka Rais Magufuli aingile kati.

"Malalamiko yetu ni kuchukuliwa maeneo yetu bila kushirikishwa, hii shule kabla ya kujengwa hapa ilikuwa katika eneo jingine, lakini sisi tuliwapa eneo kwa ajili ya kujenga... lakini wamekuwa wakiongeza mipanga mara kwa mara na kuchukua eneo letu zaidi tunaomba turudishiwe mashamba yetu walimu kazi yao kufundisha sio kulima," alisema Chitinde.

Alipohojiwa mwenyekiti wa kijiji hicho, Juma Ndoje, alikiri kuwa mgogoro huo anaufahamu na umeshafikishwa katika ngazi za juu katika ofisi ya mkuu wa Wilaya ya Bahi na yeye hana kingine cha kueleza.



Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, akizungumza wakati akihitimisha kikao cha kuvunja Baraza la Madiwani wa jiji hilo, kwa mwaka 2015 hadi 2020, jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Jiji, Godwin Kunambi na Naibu Meya, Emanuel Chibago. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wakulima ufuta waomba mfumo stakabadhi ghalani

**Na Renatha Msungu, CHAMWINO**

WAKULIMA wa ufuta katika Kijiji cha Manda wilayani Chamwino, wameiomba serikali kutoa elimu kwa wananchi juu ya mfumo wa stakabadhi ghalani, ili kumkomboa mkulima ambaye amekuwa akiangukia mikononi mwa walaguzi.

Pia, wakulima hao walidai wamekuwa wakiuza kwa walanguzi debe la ufuta kwa Sh. 15,000, huku baadhi ya madebe hayo yanayotumika yamekuwa makubwa, hivyo kuwanyonya wakulima.

Wakizungumza na waandishi wa habari, wakulima hao walisema serikali inatakiwa kujipanga kwa kutoa elimu kwa wakulima kuhusu mfumo huo wa uuzaji wa mazao kwa stakabadhi ghalani.

Mmoja wa wakulima hao, Zacharia Hansi, alisema wanatakiwa kuuza ufuta kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani, lakini tatizo lililopo ni kulipwa fedha zao baada ya wiki mbili, jambo ambalo wanaona ni usumbufu kwao.

"Serikali kama imekusudia kusaidia wakulima ingekuwa ikija huku na mizani na fedha, tunapima ufuta wanatulipa, lakini wakisema tuwauzie ufuta tusubiri malipo baada ya wiki mbili," alisema na kuongeza:

"Wakati mimi nina shida ninauza nipate fedha nitatue matatizo yangu, matokeo yake tunawauzia walanguzi ambao wanatujia na fedha na wamekuwa wakinunua debe moja kwa Sh. 15,000 hadi 18,000."

Japhet Gwisu, alisema wilaya hiyo ina ghala moja ambalo lipo kijiji cha Fufu, na wakulima hawana uwezo wa kusafiri zaidi ya kilomita 100 kufuata huduma ya ghala hilo.

"Tunalima kwa tabu na gharama kubwa kwenye ekari moja, naweza kupata gunia mbili za ufuta...leo unaniletea kwa bei yako kitu ambacho hakiwezekani, bei waliyoifikia ni Sh. 2,125, lakini watulipe fedha taslimu sio mkopo, wangekuwa wanafuatilia kwa wakulima tabu tunayopata, suala la kukopwa linatudhoofisha sana," alisema.

Haruna Javan, alitaka serikali iwakomboe wakulima kwani sasa wanauza bei ya kutupa kwa walanguzi kutokana na shida ya fedha waliyonayo.

"Mimi ufuta ninao, lakini siwezi kuuza kwa bei ya Sh. 15,000 bei hiyo bado inamnyonya mkulima, serikali ifanye kitu katika hilo," alisema.

John Mangaa, alisema serikali ina mpango mzuri ila suala la ushirika katika mkoa wa Dodoma halijatengenezewa mfumo mzuri. Alisema serikali ikae na kufikiria wakulima hasa kwenye masuala ya masoko ya mazao yao.

"Tunakodi mashamba, tunalima, tunapalilia halafu mwisho wa siku tunaambiwa tukopeshe nguvu," alisema.

Akilitolea ufafanuzi suala hilo, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga,

alisema mfumo wa stakabadhi ghalani ulikuwa na lengo la kuhakikisha mwananchi wa kawaida anapata soko zuri la mazao yake.

"Ukipata risiti unaipeleka benki na kupata fedha, lakini kinachoonekana wananchi wengi hawana elimu ya kutosha namna mfumo huo unavyofanya kazi," alisema.





# Shamba Kapunga latoa mil. 750/- kujenga kituo cha afya

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

SHAMBA la Kapunga Rise Project lililopo katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, limetoa Sh. milioni 750 kujenga kituo cha afya kilichopo kwenye Kijiji cha Kapunga ili kuwasaidia wananchi kuepukana na tatizo la kutembea umbali wa kilomita 25 kufuata huduma za afya.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kupokea cheti cha shukrani kilichotolewa na Ofisi ya Wilaya ya Mkuu wa Wilaya Mbarali kwa kutambua mchango wao wa kujenga Kituo cha Afya cha Kapunga, Ofisa Habari na Mahusiano wa shamba hilo, James Malick, alisema waliamua kujenga kituo hicho kwa gharamza zao wenyewe ili kuendelea kudumisha uhusiano baina yao na wananchi wanaozunguka shamba hilo.

Alisema hadi sasa kituo hicho kimekamilika na kinaendelea kutoa huduma za matibabu baada ya kukamilisha ununuzi wa vifaa vyote vya matibabu.

"Kutokana na mahusiano mazuri tulionayo baina ya shamba letu wananchi wa kapunga, lakini na adha wanayopata kufuata huduma ya afya maeneo mengi ambapo hutumia kilomita 25, tuliamua kujenga kituo cha afya kwenye kijiji hicho ambacho kiko kwenye kata ya Itamboleo," alisema Malick.

Akikabidhi cheti cha shukrani, Mkurugenzi wa Wilaya ya Mbarali, Kivuma Msangi, alipongeza hatua ya shamba hilo kuamua kujenga kituo cha afya, ili kuokoa maisha ya wananchi hususani wajawazito na watoto.

Aliwahamasisha wadau wengine kujitolea kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya, shule na barabara ili kuwasaidia wananchi kupata huduma bora na kwa wakati.

# Hatimaye Tanroads yakabidhi mil. 20/- wananchi Isyonje

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

HATIMAYE Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) wamekabidhi Sh. milioni 20 kwa wananchi wa Kijiji cha Isyonje, Kata Isongole, wilayani Rungwe ili kusaidia ujenzi wa shule za msingi.

Fedha hizo zilitolewa jana ikiwa ni siku moja baada ya Rais Dk. John Magufuli, kuamuru Tanroads Mkoa wa Mbeya kuchangia kiasi cha Sh. milioni 20 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Shule ya Msingi Isyonje.

Akikabidhi fedha hizo Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ambaye aliongozana na maofisa wa Tanroads, alisema fedha hizo ni utekelezaji wa ahadi ya Rais Magufuli kuwasaidia wananchi ujenzi wa shule hiyo.

"Wakati Rais Magufuli akizungumza na wananchi wa Isyoje kupitia simu yangu, aliwaahidi kuwa Tanroads watatoa kiasi cha Sh. milioni 20 kuchangia ujenzi wa Shule ya Msingi Isyoje na sasa ametimiza amenitumia mimi kuukabidhi uongozi wenu wa wilaya fedha hizi," alisema Chalamila.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Rungwe, Loema Peter, alimshukuru Rais Magufuli kwa msaada huo na kuahidi kuwa fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili ambayo yatakamilika kwa muda wa miezi minne pamoja na ununuzi wa madawati.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Naomi Mwakuka, aliahidi kusimamia ipasavyo ujenzi wa shule hiyo na kwamba nguvu kazi ya wananchi katika ujenzi wa shule hiyo utakuwa ni kipaumbele chao.

Awali, zaidi ya kaya 100 za kata hiyo ziliiomba Tanroads, kuwapa ruhusa ya kuyaendeleza maeneo yao kufuatia kuwataka kusitisha kuendeleza eneo hilo baada ya kufanyiwa tathmini ya malipo ya Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa mizani ya kisasa.

Wananchi hao walisema tangu kufanyika kwa tathmini miaka mitatu iliyopita, hawajalipwa fidia hali inayosababisha nyumba zao kuchakaa na Rais Magufuli kuamuru Tanroads kurudisha eneo hilo kwa wananchi na kutafuta eneo lingine kwa ajili ya ujenzi wa mizani.



Wafanyabiashara ndogo wa Kata ya Uyole, wakiendelea na biashara ya kuuza karoti, jirani na barabara kuu ya Tanzania na Zambia, eneo la stendi ya Usangu, jijini Mbeya jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wao. **PICHA GRACE MWAKALINGA**

# Hospitali Mbarali yaanza kutoa huduma

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

HOSPITALI ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya ambayo inajengwa baada ya Serikali Kuu kutoa zaidi ya Sh. bilioni 1.5, imekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 na tayari imeanza kutoa baadhi ya huduma kwa wananchi.

Mkurugenzi wa Wilaya ya Mbarali, Kivuma Msangi, aliyasema hayo jana wakati wa kikao cha kuhitimisha Baraza la Madiwani ambacho kiliketi kwenye Mji wa Rujewa.

Alisema kwa sasa hospitali hiyo imeanza kutoa baadhi ya huduma zikiwamo za ustawi wa jamii na wagonjwa wa nje (OPD), huku ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya (DMO) pia ikihamishiwa ndani ya majengo ya hospitali hiyo.

"Katika kipindi cha miaka mitano ya serikali ya awamu ya tano, halmashauri yetu tulianza ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya na serikali kuu ikatusaidia shilingi bilioni moja na nusu, nafurahi kuwaarifu kuwa mpaka sasa hospitali yetu imekamilika kwa asilimia 90 na tayari imeanza kutoa baadhi ya huduma kwa wananchi wetu," alisema Msangi.

Alisema ili kukamilisha kabisa ujenzi, serikali kuu hivi karibuni imewaongezea fedha Sh. milioni 300 kwa lengo la kuhakikisha miundombinu yote muhimu inayohitajika inakamilika.

Alisema fedha za nyongeza zinakusudiwa kutumika kukamilisha majengo ya maabara, mionzi wazazi, chanjo, chumba cha dawa, sehemu ya kuchomea taka ngumu na kukamilisha malipo ya wazabuni.


"Katika fedha hizo tulizoongezewa, Sh. milioni 25 zitatumika kwenye ujenzi wa jengo la mionzi, Sh. milioni 48 zitatolewa kwa ajili ya malipo ya madeni ya wazabuni na mafundi, Sh. milioni 17, tutazitumia kukamilisha jengo la maabara na pia tutajenga kichomea taka ngumu kwa Sh. milioni 27," alifafanua Msangi.

Alisema pamoja na nia njema ya serikali kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo, bado kuna mambo yanayohitajika ili wananchi wafurahie kupata huduma kwenye hospitali hiyo.

Alisema miongoni mwa mambo hayo ni kuboresha miundombinu hasa barabara zinazoelekea hospitalini hapo pamoja na kuomba mamlaka zinazohusika kuandaa usafiri wa umma utakaokuwa ukifikisha kirahisi wananchi hospitalini hapo.

"Tunakusudia kuzungumza na Tarura (Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini) ili watuboreshee barabara zetu za kuelekea kwenye hospitali ya wilaya na pia wenzetu wa Latra nao tutawaomba watupangie ruti ya daladala au bajaj zianze kupita hospitalini hapo ili kuwezesha wananchi kufika kirahisi kwenye hospitali yetu mpya na kupata huduma," alisema Msangi.

Hata hivyo, Msangi alisema kuwa pamoja na kuanza kutolewa kwa huduma kwenye hospitali hiyo, bado hospitali ya zamani pia itaendelea kutumika kwa kutoa huduma za afya kwa wananchi ambao watakwenda hapo mpaka hapo miundombinu yote muhimu itakapokamilika kwenye hospitali mpya.



## Waitwa kujiandikisha ZEC awamu marejeo

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja, Hassan Khatib, amewataka wananchi waliokosa fursa ya kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura kwa awamu ya kwanza kuijitokeza kwa wingi katika zoezi hilo la marejeo.

Hassan ameeleza hayo baada ya kumaliza ziara yake ya kukagua vituo vya uandikishaji iliyowashirikisha viongozi wa wilaya ya Magharibi 'A' katika vituo vya Regeza Mwendo na Kianga.

Alisema ni vyema kwa wananchi kutumia fursa hiyo ya kikatiba katika kushiriki kwenye zoezi hilo la uandikishaji awamu ya pili ambalo Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) imetoa siku mbili kwa kila wilaya kukamilisha kazi hiyo.

"Ni zoezi la siku mbili kwa kila wilaya, ni vyema kwa kila mwananchi mwenye sifa ambaye amekosa fursa ya kujiandikisha awamu ya kwanza, atumie nafasi hii ili kuja kupata nafasi ya kuchagua kiongozi anayemtaka," alisema Mkuu huyo wa Mkoa.

Aidha, mkuu huyo aliwapongeza wasimamizi wa vituo, wananchi na mawakala wa vyama mbalimbali vya siasa katika vituo hivyo kwa utararibu mzuri katika zoezi uandikishaji na kuimarisha amani na utulivu.

"Nimetembelea takribani vituo vitatu, lakini sijapata malalamiko yoyote kutoka kwa wasimamizi, mawakala wala wananchi," alisema na kuendelea:

"Nimeona utaratibu mzuri, na nimeelezwa zoezi linaendelea vizuri na natarajia hata uchaguzi mkuu ukifika utafanyika vyema katika mkoa wetu."

Naye Msimamizi wa Kituo cha Kianga, Abubakar Hassan Choum, alisema zoezi hilo linaendelea vizuri katika maeneo yao na wamezingatia kikamilifu miongozo na maelekezo ya Wizara ya Afya kuhusu kuepukana na maambukizo ya maradhi ya virusi vya corona.

"Kwanza tunakiri mwitikio wa wananchi katika zoezi hili ni mzuri, hakuna matatizo yeyote yaliyojitokeza... ni kesi za kawaida tu, lakini wananchi wamekuwa waelewa, wanafuata maelekezo na miongozo ya kujikinga na virusi vya corona," alisema Abubakar.

# EFD sasa kuanza kutumika mwakani

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WIZARA ya Fedha na Mipango imesema mashine za kutoa risiti za kielektroniki (EFD) zinatarajiwa kuanza kutumika mwakani.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, wakati akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Alisema matumizi ya mashine za risiti za kielektroniki yamechelewa kuanza kwa sababu mbalimbali ikiwamo kufanya utafiti kuhusu matumizi hayo pamoja na kasoro zilizojitokeza kwa baadhi ya nchi zilizokuwa zikitumia mfumo huo, ikiwamo Tanzania Bara.

Alisema maandalizi ya matumizi ya mashine hizo yamekamilika na Wizara ya Fedha na Mipango inakusudia kuanza kutumia mashine hizo mwakani, baada ya baadhi ya mambo ya msingi kukamilika.

"Mheshimiwa Spika, napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba maandalizi ya matumizi ya mashine za kielektroniki yapo katika hatua za mwisho kukamilika ...tunatarajia kuanza kutumia mashine hizo mwakani," alisema.

Alisema mashine hizo zilikuwa zianze kutumika tangu mwaka jana baada ya kubainika kuwapo kwa kasoro kubwa ikiwamo baadhi ya wafanyabiashara kufanya udanganyifu na kukataa kutoa risiti baada ya wananchi kufanya manunuzi.

Aliwataka wananchi kudai risiti wanapofanya manunuzi ya bidhaa mbalimbali na wakikataa kufanya hivyo ni sawa na kuikosesha serikali mapato.

"Tumefanya uchunguzi na kubaini moja ya eneo ambalo serikali inapoteza mapato mengi ni katika suala la risiti... wananchi wengi hawana utamaduni wa kudai risiti baada ya kufanya manunuzi ya kawaida, hivyo kuikosesha serikali mapato yake," alisema.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliitaka Wizara ya Fedha kuharakisha kupatikana kwa mashine za kielektroniki ili kuokoa mapato mengi yanayovuja.




Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu, Simai Mohamed Said (wa pili kulia), akikabidhi barakoa kwa waendesha bodaboda kwenye soko la Tunguu, ambazo ni sehemu ya vifaa mbalimbali vya kujikinga na maambukizo ya corona, vilivyotolewa na jumuiya ya Jawamama, kwa ajili ya wananchi wa jimbo hilo, jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# SMZ yaandaa mpango kupambana na corona

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema imeandaa na kutekeleza mpango mahsusi wa kujitayarisha na kupambana na ugonjwa wa Covid 19 pamoja na mpango wa kufufua uchumi baada ya athari za maradhi hayo.

Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, alisema hayo wakati akifanya majumuisho na kujibu hoja za michango ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia hotuba ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka 2020/21.

Alisema mpango huo wa kuhuwisha uchumi baada ya athari za ugonjwa wa Covid-19 unafanywa kwa ushirikiano makubwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Alisema BoT imeshaunda timu ya wajumbe kuangalia athari zilizojitokeza kutokana na ugonjwa wa Covid-19 na kuwahusisha wajumbe kutoka Zanzibar. "Mheshimiwa, athari zinazotokana na ugonjwa wa Covid-19 tayari Benki Kuu ya Tanzania imeunda timu kwa ajili ya kufanya tathmini halisi kujua waathirika na sekta zake," alisema Balozi Ramia.

Alisema miongoni mwa makundi ambayo yanakusudiwa kupewa kipaumbele kusaidiwa katika athari za ugonjwa wa corona ni wajasiriamali wa biashara mbalimbali.

Waziri huyo alizipongeza taasisi za fedha za kimataifa ikiwamo Benki ya Dunia kwa kujenga tabia ya kuiamini Zanzibar katika miradi mbalimbali inayotekelezwa chini ya ufadhili wake.

Aliitaja miradi hiyo ikiwamo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), ambapo tayari benki hiyo umeidhinisha fedha kwa ajili ya kuanza awamu nyingine, na kwamba lengo kuzifikia zaidi ya kaya 200 ambazo hazikunufaika awali.

Alisema timu ya wakaguzi wa benki hiyo walipofanya ziara yao nchini kukagua miradi ya Tasaf, wameonyesha kuridhishwa ikiwamo matumizi sahihi ya fedha kwa kaya za walengwa wa mradi huo.

"Napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawikilishi kwamba uongozi wa Benki ya Dunia umeridhishwa kwa kiwango kikubwa na matumizi ya fedha za Tasaf zinazotolewa na taasisi hiyo, ambazo zimewafikia walengwa na kukidhi malengo na matarajio yake," alisema.

Benki ya Dunia imeshaidhinisha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa Tasaf ambao unatekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia, huku ukilenga kuzinusuru kaya maskini na kujitegemea.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NAFASI ZA KAZI**

**NAFASI ZA KAZI YA DEREVA NA MAUZO** Mwenye uzoefu wa kuuza Maji. PIga simu namba : **0767 269677 saa za kazi**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## OFA

**JIPATIE VIFAA KINGA KWA BEI YA JUMLA**

**VITAKASA MIKONO**

5 LTR @ 45,000 (1PC)
40MLS @ 24,000 (24PCS)
100MLS @ 36,000 (24PCS)

**SABUNI YA KUNAWIA**

500MLS @ 21,000 (12PCS)
5 LTR @ 10,000 (1PC)

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
+255685106060
+255719834188

115772502

## KUPOTEA KWA CHETI



**REIDES OCTAVIUS PETRO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye CS No. 18064805 cha mwaka 2018 Nyaishozi Sekondari. **Index No. S.0667/0033.** Kwa yeyote atakayekiona cheti hicho awasilishe kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye au apige simu namba **0627 943 206 / 0759 424 760.** Taarifa ya polisi: **KAG/KAY/RB/442706/2020.**

115772102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**


**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;148/2020**

**Ombi la KIGUGE PILIPILI KIGUGE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu AUREA MICKY KIGODA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 06/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 10/06/2020.



115771802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Mjini Tanga.**

**Usimamizi wa Mirathi Namba 54/2020.**

**Ombi la Salehe Omari Mwabao kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu Mwanakombo Hamisi Tawfiq.**

**Kwa yeyote anayehusika.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 27/05/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 27/04/2020



115771902

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676*




**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ziwa Rukwa laleta matumaini viumbe hai

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

TAKWIMU za Ofisi ya Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa, zinaonyesha kuwa ziwa hilo limejaa na kufikia mita 7.47, Aprili, mwaka huu ikilinganishwa na mita 5.78 zaidi ya miaka 16 iliyopita na kuleta matumaini kwa viumbe vinavyoishi kwenye ziwa hilo.

Ofisa maji bodi ya bonde hilo, Grace Chitanda, alisema hatua ya kujaa maji na kufikia kiwango hicho inatokana na kiwango kikubwa cha mvua zilizonyesha mwaka huu.

Alisema vipimo vilivyofanyika ndani ya ziwa hilo vinaonyesha kuwa ziwa hilo lina wastani wa kina cha mita nne, ingawa baadhi ya maeneo yana kina cha mita tisa, tatu na nne.

Alisema kiwango mita 7.47 ni sawa na mita 813.4 za juu ya usawa wa bahari na kuwa kiasi cha maji kilichojaa kwa wastani wa mita 5.78 kwa muda mrefu katika ziwa hilo ni sawa na mita 811.7.

Alisema kumbukumbu zinaonyesha kuwa Ziwa Rukwa liliwahi kukauka na kusababisha baadhi ya viumbe ndani ya ziwa hilo kutoweka katika mwaka 1770, na mwaka 1939 ziwa hilo lilijaa ikilinganishwa na kumbukumbu za miaka yote ya nyuma.

"Ziwa hili lina maajabu kidogo, kuna mwaka liliwahi kukauka kabisa, lakini mwaka 1939, linatajwa kuwa lilijaa sana kuliko ilivyo kawaida na kuwa tangu kipindi hicho halijawahi kukauka tena," alisema Grace.

Alisema mbali na jitihada zinazofanywa za kulinda na kulihifadhi ziwa hilo na mito, kunachangamoto za kibinadamu zinazosababisha kujaa udongo kutokana na ufugaji, uchimbaji wa madini na kilimo.

Pia, uvamizi wa baadhi ya wananchi kujenga makazi karibu na ziwa.

Grace alisema ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira katika ziwa hilo, Ofisi ya Bodi ya Bonde la Ziwa Rukwa, imeunda jumuiya za watumiaji wa maji ambazo zina katiba na sheria ya kudhibiti uharibifu huo.

Alisema, ofisi hiyo pia imefanya jitihada za kutunza vyanzo vya maji na mpaka sasa kuna vyanzo 16, Jiji la Mbeya likiwa na vyanzo vinane vilivyohifadhiwa na kuna mpango wa kujenga mabwawa ya kuhifadhi maji.

Pia alisema ofisi hiyo hupima viwango vya mvua katika vituo vyake vya Utengule, Usongwe, Namanyele, Isangati na Inyonga.

Ziwa Rukwa linategemewa kwa utiririshaji maji kutoka mito ya Momba, Katuma, Songwe, Rungwa, Rwiche na Muze na utafiti wa kiwango cha udongo unaoingia ndani ya ziwa hilo unatarajiwa kufanyika muda wowote.

# Magari matatu yagongana, yaua watu wanane Mwanza

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WATU wanane wamekufa papo hapo na wengine watano kujeruhiwa,baada ya lori namba T.322 DCB lenye tela namba T.1351 DCA aina ya Scania kugonga nyuma ya tela la trekta. namba T.952.

Scania hilo lilihama njia na kugongana uso kwa uso na gari la abiria ambalo liliwabeba abiria waliokufa.

Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, ACP Murilo Jumanne, alisema ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 7:45 jioni, na kuwa watu waliokufa pamoja na majeruhi watano walikuwa wamepanda gari la abiria aina ya Hiace namba T.775 DEG Nissan iliyokuwa ikitokea jijini Mwanza likielekea wilayani Magu mkoani hapa.

Alisema tukio hilo lilitokea katika eneo la Kijiji cha Ihayabuyaga, Kata ya Bukandwe Tarafa ya Sanjo katika barabara ya Mwanza- Musoma.

Kwa mujibu wa Kamanda Murilo, miongoni mwa waliokufa ni dereva na mmiliki wa Hiace, George Philipo Msangi, mkazi wa wilayani Magu.

Murilo alisema,wanamshikilia dereva wa lori lililosababisha ajali, Boniface Cliphord, mkazi wa mtaa wa Nera wilayani Nyamagana jijini Mwanza, aliyekuwa akiendesha gari hilo kutoka wilayani Busega kwenda jijini Mwanza.

Murilo alisema waliokufa na majeruhi wote ni wanaume na kwamba miili iliyotambuliwa ni Msangi na Hamis Masige, ambaye ni mwalimu wa Shule ya Sekondari Lugeye, huku miili sita ambayo haijatambuliwa ikihifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Bugando.

Majeruhi waliolazwa Bugando ni Kasabuku Kishela (32), mkazi wa Magu, Ayubu Mindule, ambaye ni Mratibu wa Elimu Kata ya Chabula, Elias Lutandula (46), Elias Francis (44) na Edibin Makubo(28), ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha sita katika Shule ya Bariadi.

Murilo alisema Polisi inamtafuta dereva wa trekta, ambaye alitoroka, huku uchunguzi wa ajali hiyo ukiendelea.

Hata hivyo, alisainisha kuwa uzembe wa dereva wa lori ndichi chanzo cha ajali hiyo.

Muuguzi Kiongozi wa wodi ya wanaume Bugando, Lukas Alfred, alithibitisha kuwapokea majeruhi watano, na kuwa wawili wapo katika kitengo cha mifupa na watatu wapo idara ya fahamu wakiendelea na uchunguzi zaidi.

Mkuu wa mkoa wa Mwanza, John Mongella, aliwatembelea majeruhi hao na kuwapa pole, huku akilisisitiza Jeshi la Polisi kuwachukulia hatua kali màdereva wazembe ambao wanasababisha ajali.




Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongela (katikati) na Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Jumanne Murilo, wakimjulia hali mmoja wa majeruhi wa ajali ya magari matatu; lori, trekta na Hiace, iliyotokea katika eneo la Ihayabuyaga, mkoani humo juzi jioni, walipowatembelea katika Hospitali ya Bugando jana. Watu wanane walifariki na watano kujeruhiwa katika ajali hiyo.
**PICHA: ROSE JACOB**

# Mafanikio ya Magufuli miaka 5 yatajwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ametaja mafanikio kadhaa yaliyopatikana kwa miaka mitano ya uongozi wa Rais John Magufuli ikiwamo kuongezeka kwa akiba ya fedha za kigeni hadi Dola za Marekani bilioni 5.3 kinachotosheleza kwa miezi 6.1.

Kiasi hicho kimeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2015 ambapo kilikuwa Dola za Marekani bilioni 4.4 kilichotosheleza mahitaji ya fedha za kigeni za kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.3.

Dk. Mpango alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akiwasilisha bungeni mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya Mapato na matumizi kwa mwaka 2020/21.

Alisema katika mwaka 2019/20 akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha na kukidhi mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi.

"Hadi Aprili 2020, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani bilioni 5.3, kasi hiki kinatosheleza kwa kipindi cha miezi 6.1 ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 4.4 kilichotosheleza kwa kipindi cha miezi 4.3 kwa kipindi kama hicho mwaka 2015," alisema.

Alisema ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa uwekezaji wa kigeni na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi.

Aidha, alisema kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kilichofikiwa ni zaidi ya lengo la kuwa na akiba ya kutosha kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa muda wa miezi 4 na pia ni juu ya lengo la miezi 4.5 lililowekwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na lengo la miezi isiyopungua 6 kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Alisema ukuaji wa pato la Taifa umeongezeka kutoka wastani wa asilimia 6.9 kutoka 6.2 kwa mwaka 2015.

Kuhusu mapato, alisema mapato ya ndani yameongezeka kufikia Sh.Trilioni 18.5 mwaka 2018/19 kutoka Sh.Trilioni 11.0 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 69.1.

Aidha, alisema mapato ya kodi yameongezeka kutoka Sh. trilioni 9.9 mwaka 2014/15 hadi Sh. trilioni 15.5 mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 56.5.

"Vile vile, mapato yasiyo ya kodi yameongezeka kutoka Sh.bilioni 688.7 mwaka 2014/15 hadi Sh. trilioni 2.4 mwaka 2018/19 na Sh.trilioni 2.25 katika kipindi cha miezi 10 ya kwanza ya mwaka 2019/20," alisema.

Alisema ongezeko la mapato limetokana na juhudi zilizofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano kudhibiti upotevu wa mapato kwa kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi na matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji wa mapato.



# LALLANA

## LIVERPOOL SASA KIMEELEWEKA

**LIVERPOOL, England**

KIUNGO wa Liverpool, Adam Lallana, amekubali kuendelea kuitumikia klabu hiyo mpaka mwishoni mwa msimu huu kwa mkataba maalumu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 32, angeondoka huru mwishoni Juni ambapo ndio tamati ya mkataba wake wa sasa, lakini mkataba mpya utaendelea kumpa fursa ya akisalia klabuni hapo.

Msimu wa 2019-20 utaendelea Juni 17, mwaka huu baada ya mapumziko ya zaidi ya siku 100 kutokana na uwepo wa janga la virusi vya corona.

"Hii ina maana kubwa kwenye maisha yangu, nafasi niliyopewa ni ya kipekee kwangu na familia yangu pia," amesema Lallana.

Liverpool wanaongoza msimamo wa Ligi Kuu England kwa tofauti ya alama 25 kwa timu iliyo nafasi ya pili, Manchester City, kama watafanikiwa kuchukua taji itakuwa mara ya kwanza baada ya miaka 30.

Mechi ya kwanza itakuwa dhidi ya Everton Juni 21, mwaka huu wakati ya mwisho itakuwa dhidi ya Newcastle United Julai 26.

Lallana alijiunga na Liverpool mwaka 2014 akitokea Southampton ambapo alisajiliwa na aliyekuwa Kocha Mkuu, Brendan Rodgers, ambapo hivi sasa anahusishwa kujiunga nae tena Leicester City.



## ETO'O: MSIMBEZE SUAREZ KWA MARTINEZ

**BARCELONA, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Barcelona na Inter Milan, Samuel Eto'o, amemsifia Lautaro Martinez, lakini amesema Luis Suarez anastahili heshima zaidi kutokana na mchango wake.

Martinez mwenye umri wa miaka 22, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia kwa miamba hao wa LaLiga, huku fowadi huyo wa Inter akitajwa kama mrithi wa muda mrefu wa Suarez.

Sasa akiwa na umri wa miaa 33, Suarez aliwasili Camp Nou kutoka Liverpool mwaka 2014, na ameshinda mara nne taji la LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Eto'o, ambaye alitumia misimu mitano akiwa na Barca na miaka miwili kule Inter kipindi chake cha uchezaji, amesema wakati Martinez ana kipaji, mchango wa Suarez haupaswi kudharaulika.

"Nampenda Suarez, ni mmoja wachezaji bora zaidi katika nafasi yake duniani," amesema mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Cameroon akiiambia redio Katalunya Jumatano.

"Barca mara zote yupo imara, lakini wanahitaji kusimama na Luis Suarez. Katika nafasi yake ni mmoja wa wachezaji bora zaidi.

"Lautaro anafanya vizuri pale Inter na ana majaliwa mazuri ya baadaye, lakini watu wanataka kusahau haraka historia ya Luis aliyoiandika, sio tu kwa Barca, bali ni kwa historia ya soka."

# Griezmann: Naisubiri LaLiga kwa hamu

**BARCELONA, Hispania**

NYOTA wa Barcelona, Antoine Griezmann, amekuwa na muda mzuri zaidi wa kupumzika kabla ya kuendelea na LaLiga baada ya msimu kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, kuliko miaka mitano iliyopita.

Soka la Hispania pamoja na dunia yote lilisimama kutokana na mlipuko huo Machi, mwaka huu, lakini litaendelea wiki hii, ambapo Sevilla na Real Betis watafungua dimba la LaLiga baada ya miezi mitatu.

Vinara Barca watarudi kwenye kampeni yao bila mashabiki pale Camp Nou dhidi ya Real Mallorca Jumamosi na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, Griezmann hana muda wa kusubiri kurudi uwanjani.

Kikosi hicho cha Quique Setien kinaongoza kwa pointi mbili zaidi kileleni dhidi ya Real Madrid, huku zikiwa zimebakia mechi 11.

"Nafikiri kwa hali yangu binafsi, hii imekuwa likizo ndefu zaidi kwangu," amesema Griezmann akiiambia Barca TV.

"Nimekuwa na wakati wa kupumzika. Nafikiri ni zaidi ya miaka mitano iliyopita ndio safari hii nimepata muda wa kupumzika mrefu zaidi kiakili na kimwili.

"Nilikuwa na wakati wa kupumzika na familia yangu, watoto wangu na sasa nipo tayari kwa ajili ya mapambano."




# SARRI: NI NGUMU RONALDO NA DYBALA KUWACHEZESHA PAMOJA

**TURIN, Italia**

NI ngumu kuwachezesha kwa pamoja Cristiano Ronaldo na Paulo Dybala, kwa mujibu wa kocha wa Juventus, Maurizio Sarri.

Baada ya kumsajili kwa euro milioni 112 mshindi mara tano wa Ballon d'Or, Ronaldo, kukasababisha Dybala umuhimu wake kwa kikosi hicho cha Bianconeri kutokuwa mkubwa msimu wa 2018-19.

Alifunga mabao 26 katika mashindano yote msimu wa 2017-18 huku akifunga 10 tu katika msimu uliofuata, huku akihusishwa na mpango wa kutakiwa Manchester United.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina bado hajafikia ubora wake chini ya Sarri, wakati Ronaldo amefunga mabao 21 kwenye Serie A kwa msimu wa pili mfululizo.

Sarri ameonekana kuwa na wakati mgumu wa kuwapanga pamoja katika kikosi chake, ingawa ameikubali changamoto hiyo.

"Dybala ni mchezaji wa kiwango cha juu. Suala la kuwafanya wacheze pamoja na Cristiano ni ngumu mmoja kutamba zaidi, kwa sababu siyo rahisi kuwafanya wacheze pamoja," amesema Sarri akiiambia Sky Sport Italia.

"Lakini kama wachezaji wawili wenye ubora kama wao wakiwapo, wachezaji wengine wanatakiwa kuzoea."

# Coman atangaza kutomhofia Sane




**MUNICH, Ujerumani**

KINGSLEY Coman amesisitiza hana tatizo na ujio wa Leroy Sane kwenye kikosi cha Bayern Munich na kwanba hana hofu ya kugombea namba.

Sane amekuwa akiwaniwa kwa muda mrefu na Bayern, huku winga huyo wa Manchester City akiripotiwa akitaka kwenda kwa miamba hao wa Bundesliga.

Na kuna uwezekano mkubwa wakati wa dirisha la usajili la majira ya joto likifunguliwa akasajiliwa na Munich, licha ya kuwa nje ya dimba tangu Agosti mwaka jana baada ya kuumia goti kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Liverpool.

Rais wa Bayern, Herbert Hainer, ameonyesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ambaye amebakiwa na mwaka mmoja na mkataba wake pale City.

Ujio wa Sane pale Munich utawafanya Serge Gnabry na mchezaji mwenzake wa Ufaransa, Coman kuwa na wakati mgumu wa kugombea namba kwa pamoja.

"Wakati nikija hapa Bayern Munich tulikuwa na Franck Ribery, Arjen Robben, Douglas Costa na mimi, na nilikuwa bado mchezaji kijana, ikilinganishwa na magwiji Ribery na Robben," amesema Coman akiliambia jarida la Bild.

"Unaweza kuona sikuwa na tatizo, ni suala bora kwa timu kuwa na wachezaji wengi wenye viwango vya juu.

"Kama Sane akija, hakutakuwa na tatizo! Isipokuwa kama timu itasema hainihitaji tena mimi, lakini klabu inajua nilichonacho na ninachokitoa kwao."



## WALCOTT AIPA PIGO EVERTON

**LONDON, England**

FOWADI wa Everton, Theo Walcott amefanyiwa upasuaji na atakosa kipindi cha msimu wa Ligi Kuu England kilichobakia.

Walcott aliumia kwenye mazoezi wakati Everton ikijiandaa kuwavaa Liverpool pale Goodison Park Juni 21, mwaka huu.

Anatarajiwa kuwa nje ya dimba kwa kipindi cha wiki nne, hivyo hataweza kucheza kwa kipindi cha msimu kilichobaki.

"Fowadi wa Everton mwenye umri wa miaka 31 amefanyiwa upasuaji Jumatatu jioni kwenye mguu, baada ya kuumia kwenye mazoezi," ilithibitisha taarifa ya klabu hiyo.

"Ameanza kujiuguza kwa sasa na timu yetu ya madaktari inaendelea kumfuatilia kwa karibu sana."

Walcott, ambaye amecheza mechi 21 za Ligi Kuu msimu huu, alituma ujumbe wa shukrani kwenye mtandao wa kijamii.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MAN UNITED, INTER ZAMGOMBEA TALISSO

●●●Lakini inaelezwa United tayari wameshafikia makubaliano na wawakilishi wa kiungo huyo wa zamani...

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United na Inter Milan zinatajwa kuanza mchakato wa kuwania saini ya kiungo wa vigogo wa Ligi Kuu Ujerumani, Bayern Munich, Corentin Tolisso.

Kwa mujibu wa mchambuzi wa michezo wa RMC, Mohamed Bouhafsi, vinara hao wa Bundesliga wameweka wazi wako tayari kumuuza Tolisso, ambaye walimsajili katika majira ya joto mwaka 2017 kwa dau la pauni 37 akitokea Lyon.

Mchambuzi huyo alisema Manchester United na Inter Milan ni baadhi ya klabu ambazo zimeonyesha nia ya kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 25.

Bayern Munich yenyewe imejipanga kupokea pauni milioni 31, ili kumuuza kiungo huyo Mfaransa ambaye kiasi hicho cha fedha kimetajwa katika orodha ya wachezaji wanaouzwa na klabu hiyo.

Inaaminika kuwa United maarufu Mashetani Wekundu tayari wameshafikia makubaliano na wawakilishi wa Tolisso ili kukamilisha mchakato huo.

Tangu alipotua Bayern miaka mitatu iliyopita, kiungo huyo mwenye umri wa miaka 25, amefunga mabao 14 na kutoa pasi za mwisho 12 kwenye mechi 68 alizocheza za mashindano mbalimbali.

Licha ya kufanya vizuri, Tolisso alikumbana na changamoto ya kuumia mguu na hivyo kucheza mechi mbili tu za msimu wa 2018/19 kutokana na kufanyiwa operesheni.

Huku Tolisso akionekana anajiandaa kuondoka Allianz Arena yatakapoanza majira ya joto, inaonekana pia kama tayari ameshacheza mchezo wake wa mwisho akiwa na Bavarians.

## KWA UFUPI

**SANCHO BEI JUU**

BORUSSIA Dortmund itahitaji kulipwa kiasi cha pauni milioni 115 ili kumuuza winga wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, ambaye ana umri wa miaka 20. ***(Telegraph)***

**ZAHA ANUKIA PSG**

MSHAMBULIAJI wa Crystal Palace ambaye ni raia wa Ivory Coast, Wilfried Zaha (27), ametajwa kuwavutia mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Paris St-Germain. ***(90 Min)***

**CHELSEA, MADRID VITANI**

CHELSEA itakutana na ushindani dhidi ya Real Madrid katika mchakato wa kuwania saini ya kiungo wa Bayer Leverkusen na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Kai Havertz, ambaye ana umri wa miaka 21. ***(Sun)***

**GERSON ANUKIA CHELSEA**

CHELSEA inajiandaa kufanya mchakato wa kumsajili kiungo wa Flamengo Mbrazili Gerson (23), katika dili ambalo litaifaidisha pia klabu yake ya zamani ya Roma. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

**COUTINHO KUREJEA EPL**

KIUNGO wa Barcelona, Philippe Coutinho, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Bayern Munich, anaonekana kuwa kwenye nafasi kubwa ya kurejea kwenye Ligi Kuu England. Tottenham, Everton na Newcastle zinatajwa kuwania saini ya Mbrazili huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(France Football - in French)***

**MOURINHO AMTAKA GIROUD**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho anataka kumsajili straika wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Olivier Giroud, ambaye ana umri wa miaka 33. ***(Express)***

**CLARK KUMRITHI CHILWELL**

LEICESTER City imeweka wazi itamsajili beki wa kushoto wa Vitesse Arnhem, Max Clark (24), kwa ajili ya kuchukua mikoba itakayoachwa na Ben Chilwell (23), kama beki huyo wa Timu ya Taifa ya England ataamua kuondoka klabuni hapo. ***(Mail)***

**BERTRAND MAMBO SAFI**

MABOSI wa Southampton wanapanga kufanya mazungumzo kwa ajili ya kumpa mkataba mpya beki wake wa kushoto, Ryan Bertrand (30), ambaye anawania na Foxes. ***(Mail)***

**BOURNEMOUTH YAJIPANGA**

GOLIKIPA wa Bournemouth, Artur Boruc (40), kiungo, Andrew Surman (33), mabeki, Simon Francis (35), na Charlie Daniels (33), wanajiandaa kusaini mikataba mingine mipya mifupi na klabu yao hiyo. ***(Bournemouth Echo)***

**FRASER AGOMA KUSAINI**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Scotland, Ryan Fraser (26), anajiandaa kukataa kusaini ofa ya muda mfupi ya Cherries, na uamuzi huo utamfanya ifikapo majira ya joto aondoke akiwa mchezaji huru. ***(Sun)***

**HUGHTON AKWAMA**

INAELEZWA nafasi ya Kocha, Chris Hughton kurejea kuifundisha Birmingham ni ndogo. ***(Birmingham Mail)***

**UNITED, WEST KUJIPIMA**

MANCHESTER United itacheza mara mbili dhidi ya West Brom kwenye Uwanja wa Old Trafford leo ili kujiandaa kuelekea kurejea kwa Ligi Kuu England. ***(Telegraph)***

HABARI MICHEZO

# SIMBA YAIPIGA 'KIJEMBE' YANGA IKITESEKA NJIANI

**Na Faustine Feliciane**

UTANI wa jadi wachukua nafasi, ndivyo unavyoweza kusema baada ya Simba 'kuwapiga dongo' watani zao baada picha kusambaa ikionyesha basi la Yanga lililobeba kikosi cha timu hiyo kuharibika wakiwa njiani kuelekea Shinyanga.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema timu inayofanya mabadiliko inatakiwa ijiwekee 'ukubwa' wa timu yao na kutokubali kufanya mambo ya kushusha taswira ya klabu.

"Timu inajiita kubwa inafanya mabadiliko halafu wachezaji wanasafiri kwa basi kwa umbali mrefu tena kwa basi lililochoka, wanafika sehemu linaharibika, wanafika mbele wanasimama kununua mahindi au mayai, haiwezekani," alisema Manara.

Kiongozi huyo alisema Yanga wanapaswa kuiga kutoka kwao (Simba), ambao hawakubali timu isafiri kwa njia ya barabara katika umbali wa zaidi ya kilometa 300.

"Simba inaonyesha kwa vitendo ukubwa wa timu yao, haikubali wachezaji wasafiri zaidi ya kilometa 300 kwa kutumia basi, zaidi ya kilometa hizo ni ndege tu, hiyo ndio maana ya timu kubwa," Manara alisema.

Manara alisema pia kitendo cha mchezaji wa Yanga (David Molinga), kupiga simu katika kituo cha redio na kulalamika moja kwa moja, hali hiyo inaonyesha timu hiyo ina udhaifu au ni yenye hadhi ya chini.

"Simba huwezi kukuta Chama (Clatous), anapiga simu redioni kulalamika, mambo ya timu yanamalizwa ndani ya timu kwa taratibu za timu, hiyo ndio maana ya timu kubwa, timu kubwa ni vitendo sio porojo," aliongeza Manara.

Kauli hiyo ya Manara imekuja siku moja baada ya Molinga kulalamika kwenye kituo kimoja cha radio alikataa kusafiri na kikosi cha Yanga kuelekea Shinyanga kwa sababu hakuwa kwenye mipango ya kocha, jambo ambalo lilikanushwa na viongozi wa klabu hiyo.




Beki wa Coastal Union, Haji Ugando, akipiga danadana katika mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Disuza, Tanga jana, kwa ajili ya kujiandaa na mechi dhidi ya Namungo itakayochezwa kesho jijini humo. **PICHA : OSCAR KASIMIRI**

# Beki Simba amfunda Mwamnyeto

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA beki wa Simba, Fikiri Magoso, amemtaka mlinzi wa Coastal Union, Bakari Mwamnyeto, kujitambua endapo atapata nafasi ya kusajiliwa na moja ya vigogo wa soka nchini, Simba au Yanga.

Mwamnyeto ametajwa kuwindwa na klabu hizo na sasa kinachosubiriwa ni kufunguliwa rasmi kwa dirisha la usajili.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Magoso alisema Mwamnyeto ni mchezaji anayetegemewa katika kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), hivyo anatakiwa kujituma na kujihakikishia nafasi ya kucheza kama ataondoka Coastal Union.

Magoso alisema amemfuatilia kwa muda mrefu beki huyo na kuweka wazi amekuwa ni msaada mkubwa kwenye kikosi cha Taifa Stars cha sasa na hata hapo baadaye kutokana na umri wake kuwa mdogo.

"Kwa upande wangu ninavyomwona Mwamnyeto ni kizazi cha zamani ambacho kimeibuka sasa, ila anatakiwa kuwa makini, kujituma pale atakaposajiliwa katika moja hizo timu," alisema Magoso.

Alimtaka mchezaji huyo kutoridhika mapema kwa sababu anaweza akapoteza namba yake kwenye kikosi cha Stars baada ya kusajiliwa katika timu kongwe.

"Kwa upande wangu natamani kumwona Mwamnyeto akicheza Simba, akipata bahati ya kusajiliwa katika kikosi cha timu hiyo, anatakiwa kupambana ili asije kupoteza nafasi yake Stars, wachezaji wengi wazawa wanajisahau wanaposajiliwa na hizi timu kubwa, wanashindwa kufanya vizuri na kupoteza ubora wao, nahitaji kumwona anafika mbali zaidi," alisema Magoso.

Klabu ya Coastal Union imetaja thamani ya Mwamnyeto kuwa ni Sh. milioni 100, na ikieleza Yanga ndio wamefika rasmi kwa ajili ya

mazungumzo ya kumsajili beki huyo.

## Mbao yajipanga kuiadhibu Azam

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mbao FC, Abdulmutik Haji, amesema mbinu pekee itakayowabakisha kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ni kupambana na kushinda mechi zao zote zilizobakia bila kujali wanacheza nyumbani au ugenini.

Haji aliliambia gazeti hili ili wajihakikishie kubakia kwenye ligi, wanahitaji kupata matokeo chanya katika mechi hizo za hatua ya lala salama.

Kocha huyo alisema wamejipanga kuongeza umakini ili malengo waliyonayo ya kujinasua na janga la kushuka daraja yaweze kutimia.

Alisema wamefanya maandalizi mazuri kuelekea mchezo wao wa kwanza dhidi ya Azam FC utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini.

"Tunakazi ngumu ya kucheza mechi tisa zilizobaki, mechi zote ni ngumu, tunahitaji kujiandaa na kupambana na wapinzani wetu, iwe nyumbani au ugenini, malengo yetu ni kutafuta matokeo mazuri ili kubaki kwenye mikikimikiki ya ligi msimu ujao," alisema Haji.

Aliongeza timu yake iko kwenye nafasi mbaya katika msimamo wa ligi, hivyo wanalazimika kupambana na kucheza kwa kasi ya kiwango cha juu.

"Azam ni wazuri, hatuwadharau wapinzani wetu, lengo kubwa ni kupambana tunaenda kupata ushindi katika mchezo huo na mingine itakayofuata mbele ili kubakia katika ligi msimu ujao," alisema kocha huyo.

Mbao ipo katika nafasi ya 19 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 22.

## Taifa Jang'ombe yaiwaza Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKATI bado ikisubiri ruhusa ya serikali ili kuendelea na Ligi Kanda ya Unguja, Kocha Mkuu wa Taifa Jang'ombe, Mohamed Ali 'Shaxi' amesema bado lengo la timu hiyo ni kupambana na hatimaye kusaka nafasi ya kupanda daraja.

Taifa Jang'ombe ndio kinara katika Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja wakiwa na alama 34 huku wakiwa wamebakisha michezo sita mkononi ili kukamilisha ratiba ya ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Shaxi alisema kikosi chake kinaendelea kujiimarisha na kuwa tayari kuendelea na kampeni yao endapo serikali itaruhusu kurejea tena kwa ligi hiyo.

Shaxi alisema ili kuhakikisha wachezaji wake wanakuwa imara na 'fiti' kukabiliana na ushindani katika mechi zilizobakia, wanaendelea kufanya mazoezi huku wakijikinga na maambukizo ya virusi vya corona.

"Wachezaji wanafanya mazoezi wao binafsi kwa sababu bado tunaendelea kusubiri tamko la ligi yetu kurejea tena, iwapo serikali itaruhusu, na mimi nimekuwa nikiwatembelea mchezaji mmoja mmoja ili kuangalia jinsi gani wanafuata na kuzitekeleza programu nilizowapatia kwa kutumia njia ya mtandao," Shaxi alisema.

Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja inashirikisha timu 13 na kanuni zinasema klabu nne zitashuka daraja na tatu zitapanda kutoka katika mikoa mitatu ya kanda hiyo.

# Michezo

Ijumaa Juni 12, 2020

Nipashe


## Man United, Inter zamgombea Talisso




# Mkude kurejea dimbani mapema

**Faustine Feliciane na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wamesema kiungo wa timu hiyo, Jonas Mkude hajavunjika na anatarajiwa kuanza mazoezi hivi karibuni.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara alisema vipimo vya mwisho vya uchunguzi alivyofanyiwa Mkude vimeonyesha hajavunjika wala kupasuka eneo lolote.

"Mkude yupo kambini akiendelea na matibabu, anauvimbe kidogo ambao tayari ameanza matibabu na anaendelea vizuri na ndani ya siku mbili hizi ataanza mazoezi na wenzake," alisema Manara.

Alisema kwa sasa kumekuwa na ushindani mkubwa wa namba katika kikosi cha Simba na kila mchezaji anapambana kupandisha kiwango chake hasa ukizingatia msimu wa ligi unaelekea ukingoni.

"Unajua hiki ni kipindi ambacho wachezaji wanataka kuona wanabaki kwenye timu katika msimu ujao, kwa hiyo ushindani wa namba ni mkubwa sana, kila mchezaji anataka kucheza kuonyesha kile alichonacho," alisema Manara.

Alisema kwa kutambua hilo, Mkude ameamua kubaki kambini kutibiwa mpaka apone ili arudi uwanjani mapema kuisaidia timu yake kufikisha malengo.

Kiongozi huyo aliongeza Simba imejipanga kupambana ili kuhakikisha msimu huu wanatimiza makombe 56.

"Kwa sasa kwenye kabati letu kuna makombe 54, hivyo tunayataka hayo mawili ili tufikishe 56, na kwa uwezo wa Mungu na mikakati yetu, tutachukua ubingwa wa Bara kwa mara ya tatu mfululizo na tutachukuwa pia FA, hao wanaopiga kelele kwamba FA Kombe lao wasahau, sasa vijana wako fiti na tayari kwa ajili ya kwenda kuwapa furaha mashabiki wao," alisema Manara.

Ofisa huyo aliongeza atakuwa tayari kuachia nafasi yake ndani ya klabu hiyo siku Yanga itakapochukua ubingwa na tayari ameanza kumwandaa mrithi wake.

Kuhusu kukwama kwa kiungo wao, Sharraf Shiboub, alisema wameanza kufanya jitihada za kutafuta njia nyingine ili nyota huyo arejee nchini kuendelea na kazi yake.



Mkurugenzi wa Utawala na Uendeshaji wa Kampuni ya SportPesa Tanzania, Abbas Tarimba, ambaye aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Yanga ya jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**.

# TARIMBA AFUNGUKA KERO ZA MABADILIKO

## ●●● Asimulia alivyoitwa Ikulu kuhojiwa baada ya kundi la Yanga Asili kumshtaki wakipinga...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI Yanga ikiwa imeanza safari ya kuelekea kwenye mabadiliko, Mkurugenzi wa Utawala wa Kampuni ya SportPesa Tanzania, Abbas Tarimba, amesema aliwahi kushtakiwa kwa kiongozi mkuu wa nchi wakati akisimamia mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji wa klabu hiyo.

Mwenyekiti huyo wa zamani wa Yanga, Tarimba, alisema alikutana na upinzani kutoka katika kundi maarufu la Yanga Asili lililokuwa linapinga mabadiliko hayo ambalo liliongozwa na marehemu, Yusuph Mzimba.

Tarimba alisema hata hivyo hakukata tamaa na kila wakati aliendelea kuratibu mikutano mbalimbali ya kuelimisha wanachama na hatimaye sasa klabu hiyo imeamua kuanza upya mchakato huo.

"Mimi nilipelekwa hadi Ikulu kwa ajili ya kusimamia mabadiliko ya mfumo, nilikutana na ushindani mkubwa kutoka kwa baadhi ya wanachama ambao walikuwa wanauelewa tofauti, lakini kwa kushirikiana na wenzangu tulikuwa tunajaribu kutoa elimu ya kile tunachokitambulisha," alisema Tarimba.

Alifunguka kuwa yeye ndiye mwanzilishi wa jina la Mnyama kwa sababu chini ya uongozi wake alipata mafanikio zaidi kila walipocheza na watani zao Simba.

"Katika kipindi changu nilipata mafanikio sana hasa dhidi ya Simba, sisi furaha yetu hata kama tumfunge nani, lakini kama hatukuweza kumfunga Simba, wala hakuna raha, usisikie masuala ya twende Afrika (Ligi ya Mabingwa Afrika), lakini heshima yetu ni kuifunga Simba, kwetu sisi Simba si maadui, ni marafiki zetu," alisema Tarimba.

Alisema siku Yanga ikitoka sare na Simba, hali huwa si shwari kuanzia barabarani hadi majumbani na aliongeza mpira bila ushindani, hakuna mpira.

"Simba si maadui ila ni washindani wetu, hebu angalia siku Yanga ikifungwa au ikitoka sare, hata majumbani hali inakuwa si shwari, mpira bila ushindani, hakuna mpira, hata nchi zilizoendelea utakuta kuna timu mahasimu, kama Manchester United ikicheza na Manchester City, si unajua panavyochimbika, hii inaleta ushindani kweli kweli," Tarimba alisema.

Alisema yeye haamini vitendo vya ushirikina na alipokuwa kiongozi wa Yanga alitoa ushirikiano kwa 'kamati za ufundi' ili kusaidia ushindi kwa sababu ni sehemu ya mila na tamaduni za Afrika.

"Miaka ya nyuma, enzi zetu zile, mabasi, watu wamebadilisha nguo zao na ukienda kwenye miti, bendera zimetanda, ile ilikuwa inaleta haiba kubwa kwenye mpira, wanaoroga ndio usiseme...lazima tuwe wakweli, sisi tuko Afrika, haya mambo yako kwenye asili, kweli si kweli, Mungu anajua," aliongeza kiongozi huyo.

Alisema pia alipokuwa kiongozi wa timu hiyo walikuwa wakijiridhisha na kikosi kinachopangwa kabla ya mchezo kulingana na uzito wa mechi husika.

"Kwa nia njema kabisa, wataalamu wa soka wanaweza waseme mwalimu asiingiliwe, lakini sisi kama viongozi timu inapofungwa, balaa liko kwetu, mwalimu anaenda kukaa hotelini, suala sio kutomwamini mwalimu, ni kujiridhisha," aliongeza Tarimba.

Hivi karibuni, uongozi wa Yanga kwa kushirikiana na wadhamini wao, Kampuni ya GSM, walisaini mkataba na LaLiga kwa ajili ya kuwasaidia mwongozo wa kuelekea kwenye mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >